SportPesa
TZS. 735,865,580
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



UKURASA 3

**MVUA kubwa ya siku tatu yaja mikoa 6**




UKURASA 11


# Nipashe

Jumamosi Desemba 4, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580784

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Rais Samia: Machinga hamtajuta kuhama

**ASEMA** ni jambo lake, awaahidi mambo mazuri... *Endelea ukurasa wa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akiwasikiliza wataalamu mbalimbali wa kiwanda cha kutengeneza nyaya za mawasiliano cha Raddy Fiber Manufacturing Tanzania Ltd alipotembelea maabara ya kupima uwezo wa nyaya baada ya kuzindua kiwanda hicho wilayani Mkuranga mkoani Pwani jana. **PICHA: IKULU**

UKURASA 2

# Ma-RC, ma-DC wapewa jukumu chanjo ya corona




Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, akipokea hati ya makabidhiano ya shehena ya dozi 115,200 za chanjo ya UVIKO-19 ya Johnson kutoka kwa Balozi wa Ubelgiji nchini, Peter Van Acker, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam jana, zilizotolewa na serikali ya nchi hiyo kupitia mpango wa COVAX.
**PICHA: JAMES KANDOYA**

UKURASA WA 4

## BASTOLA YATELEKEZWA CHOONI

WAKATI Jeshi la Polisi likifuatilia utekelezaji wa agizo la serikali kuwataka wote wanaomiliki silaha kinyume cha sheria kuzisalimisha, mkoani Morogoro bastola...





UKURASA WA 4

## JESHI LA ZIMAMOTO LAOKOA KICHANGA ALIYETUPWA CHOONI

MTOTO mchanga, ameokolewa akiwa hai kutoka katika shimo la choo cha shule ya msingi..

# Wanaume wafanyiwa upasuaji wa matiti

UKURASA 2

MICHEZO SIMBA YAFUNGUKA INAKWENDA VITANI UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6

# Samia: Machinga hamtajuta

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema machinga hawatajutia uamuzi wa serikali wa kuwahamishia kwenye maeneo maalumu, akiahidi kuwa mambo mazuri yanafuata kwa wafanyabiashara wadogo hao.

Aliitoa ahadi hiyo jana mbele ya wananchi wakati akiwa eneo la Vikundi wilayani Mkuranga mkoani Pwani.

Rais Samia alisema kuwa suala la machinga ni lake na kuwaomba wampe muda, akisisitiza kuwa hawatajuta kwa kuwa atahakikisha wanajiajiri sehemu nzuri zenye huduma zote.

Mkuu wa nchi alikwenda Mkuranga kuzindua kiwanda cha kutengeneza nyaya za mawasiliano cha Raddy Fiber Manufacturing na alipofika Vikindu alisimama na kutoa ahadi hiyo kwa machinga.

"Nimeona vidole vya vijana vipo juu, nadhani wanataka kuzungumzia suala la machinga, hilo suala ni langu, ni mradi wangu binafsi na hilo ninataka kuwaahidi mazuri kwenye hilo.

"Nipeni muda, kubalini ya sasa hivi, hameni, nendeni mnakopangishwa, ninataka kuwaahidi kwamba hamtajuta, mimi na halmashauri tutafanya kazi kuhakikisha vijana wetu wanajiajiri sehemu nzuri, sehemu zenye huduma zote, wanafanya kazi saa 24 kwa wale watakaoweza, hamtajuta ndugu zangu," alisisitiza.

Rais Samia alisema upo mradi mkubwa ambao kwa sasa anazungumza na ulimwengu ili kuzikopesha halmashauri moja kwa moja na hizo fedha zitatumika kujenga maeneo ya machinga.

"Ninaomba mniamini, ninaomba mniachie, tupeni muda tulifanyie kazi, mambo yatakuwa mazuri," Rais alisema.

Akizindua kiwanda hicho cha nyaya, Rais Samia alisema serikali inatambua mchango wa sekta binafsi katika kuleta mageuzi makubwa ya kiuchumi, hivyo itaendelea kuweka mazingira wezeshi na rafiki ya kufanyia biashara na uwekezaji.

Alitumia fursa hiyo kuwakaribisha wawekezaji wengine kutoka ndani na nje ya nchi kuwekeza Tanzania na kuwahakikishia usalama wa mitaji yao pamoja na uhakika wa kutengeneza faida.

Rais alimpongeza mwekezaji wa kiwanda hicho, Ramadhani Mlanzi, ambaye ni mzawa kwa kuona Tanzania ni sehemu salama ya kuwekeza.

Alisema uzinduzi wa kiwanda hicho unathibitisha uwezo na fursa nyingi ambazo nchi imejaliwa kuwa nazo ili zitumike kukuza uchumi, kuleta ajira hususan kwa vijana na kuzalisha bidhaa ambazo siyo lazima kuagizwa nje.

Rais Samia aliziagiza taasisi zote za serikali zinazotoa huduma katika sekya ya uwekezaji, kuondoa urasimu ambao unasababisha kupoteza baadhi ya wawekezaji waliokuwa na nia ya kuwekeza Tanzania.

Alisema serikali itaimarisha jitihada za mageuzi ya kisera na kisheria ikiwamo utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara.

Pia alimtaka Mtendaji Mkuu wa kiwanda hicho kukamilisha azma yake ya kujenga kiwanda cha kuzalisha simu janja ambacho uwapo wake utachangia ajira kwa vijana.

Kiwanda hicho kina uwezo wa kuzalisha kiasi cha kilometa 24,000 za Optic fiber kwa mwaka na kinatarajiwa kutoa ajira zipatazo 670 kitakapokamilika katika awamu zote, hivyo kukifanya kuwa kiwanda cha tatu kwa ukubwa barani Afrika na cha kwanza Afrika Mashariki na Kati.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla (wa nne kushoto), akipokea vifaa vya usafi ikiwemo vya kuhifadhi taka na mifagio kutoka kwa Jumuiya ya Mabohora ikiwa ni moja ya kuunga mkono kampeni ya kusafisha na kupendezesha Mkoa huo, jana. Kushoto kwake ni Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Murtaza Adamjee. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# Ma-RC, ma-DC wapewa jukumu chanjo ya corona

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, ameagiza wakuu wa mikoa na wilaya kwenda kwenye jamii na kushiriki kampeni za kuongeza uelewa ili kasi ya watu kuchanja iongezeke.

Dk. Dorothy alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam mara baada ya kupokea dozi ya chanjo 115,200 aina ya Johnson & Johnson kutoka Ubelgiji kupitia mpango wa Covax Facility.

Alisema hiyo ni mara ya kwanza Tanzania kupokea dozi za UVIKO-19 kutoka Ubelgiji baada ya zile za kutoka Marekani na China.

"Ninaagiza wakuu wa mikoa na wilaya wote kutoka ofisini kwenda kushiriki kwenye kampeni za kuongeza uelewa ili kuongeza kasi ya uchanjaji," alisema.

Dk. Dorothy aliwataka viongozi hao wahakikishe jamii inafuata taratibu zote za afya ikiwamo kuvaa barakoa, kunawa mikono na kufuata afua nyingine zinazoshauriwa na wizara.

Aliongeza kuwa lengo la serikali ni kuhakikisha asilimia 60 ya Watanzania wanachanjwa na mpaka sasa serikali imepokea dozi 4,421,540 zikihusisha chanjo za Sinopharm, Pfizer na Johnson & Johnson.

Hata hivyo, waziri huyo alibainisha kuwa dozi zilizopo zinatosha kuwachanja Watanzania 2,888,545 pekee.

Kiongozi huyo aliwaomba wadau wengine wa maendeleo kuunga mkono juhudi zilizofanywa serikali za Marekani, China na Ubelgiji kusaidia upatikanaji wa chanjo za UVIKO-19 nchini.

## Wanaume wafanyiwa upasuaji wa matiti

**Na Mwandishi Wetu**

KATI ya wanaume 10 hadi 15 kwa mwaka wamekuwa wakijitokeza katika hospitali ya Aga Khan, jijini Dar es Salaam ili kufanyiwa upasuaji wa matiti.

Daktari Bingwa wa Upasuaji kutoka hospitali ya Aga Khan, Aidan Njau, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumzia kambi ya sita ambao wamenufaika na upasuaji wa bure wa kurekebisha makovu ya majeraha ya moto, ajali na wale waliokatwa titi kutokana na saratani.

Kambi hiyo imewezesha kufanya upasuaji kwa wagonjwa 24 wanawake na watoto kwa muda wa siku tatu hospitalini hapo na kufanya mpaka sasa wanufaika wa upasuaji wa bure wa kurekebisha makovu kufikia 240.

Upasuaji huo wa wagonjwa 24 umehusisha timu ya wataalamu kutoka Aga Khan kwa kushirikiana na wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) chini ya mhisani ambaye ni Shirika la Kimataifa la Reconstructing Women International (RWI) kutoka Marekani. Akizungumzia upasuaji wa wanaume kurekebisha matiti iliyoanza hospitalini hapo miaka mitano iliyopita, Dk. Njau alisema kwa mwaka wanaume wanaojitokeza huwa kati ya 10 hadi 15 na wanawake huwa kati ya 15 hadi 20.

"Tulivyoanza idadi ilikuwa ndogo, kwa mwaka walijitokeza mpaka watatu, mpaka sasa idadi yao kwa ujumla waliofanyiwa upasuaji kwa wanaume na wanawake wanafikia 30," alisema.

Kuhusu huduma za upasuaji za wagonjwa 24 zilizofanyika, Dk. Njau alisema shirika hilo la RWI linawasaidia siyo tu kutibu matatizo hayo pia kuwajengea uwezo wataalamu wazawa wa hospitali hizo mbili kuweza kuzifanya.

Alisema katika upasuaji uliofanyika kipindi hiki wamerekebisha matiti ya wanawake watatu akiwamo ambaye alikatwa kutokana na saratani.

"Tunarekebisha wa aina tofauti kulingana na hali ilivyo, yupo mama ambaye alikaa muda mrefu na titi likiwa limekatwa na ameteseka katika jamii kukubalika, ilimsumbua kisaikolojia.

"Tumechukua sehemu ya nyama tumboni kwake tukazitengeneza likawa kama titi na kuliweka eneo alilokatwa awali kwenye titi na imekaa vizuri na anaendelea vizuri yupo wodini, leo (jana) ni siku ya kwanza tangu tumfanyie upasuaji."

Daktari Bingwa wa Upasuaji kutoka Muhimbili, Edwin Mrema, alisema wanafurahi kuwasaidia watu wanaotoka kwenye vipato vya chini ambao hawajui pa kwenda.

"Hii ni fursa kwa wanafunzi wetu wenye Shahada ya Uzamili kutoka Chuo cha Tiba na Afya Muhimbili (MUHAS) na kuwajengea kujifunza zaidi kuhusiana na aina hii ya upasuaji," alisema.

Daktari Andrea Pasic kutoka shirika la RWI alisema hiyo ni kambi yao ya sita tangu kufanya upasuaji hospitalini hapo ambapo mpaka sasa waliofanyiwa kwa wanawake na watoto wanafikia 240.

"Hii ni kambi ya nne ya upasuaji wa kubadili na kuboresha viungo. Tumeweka mkazo kwa wagonjwa kutoka nje ya Dar es Salaam ambao wanaletwa hapa na wanafanyiwa upasuaji," alisema.

## HABARI KITAIFA




Wananchi wakiangalia daladala inayofanya safari zake kati ya Tabata Segerea na Mbezi kupitia Maramba Mawili, lililopata ajali na kuingia mtaroni, eneo la Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam jana. Kwa mujibu wa mashuhuda walisema baadhi ya wapita njia waliumia katika ajali hiyo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mvua kubwa ya siku tatu mikoa 6

**Na Faustine Feliciane**

MVUA kubwa inatarajiwa kuikumba mikoa sita katika kipindi cha siku tatu kuanzia leo kwa mujibu wa taarifa ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).

Mamlaka hiyo ilitangaza jana kuwa kuanzi leo mpaka Jumatatu kuna uwezekano mkubwa wa kuwapo kwa mvua kubwa ambayo inaweza ikaleta madhara kwa wananchi wa maeneo hayo.

Mikoa iliyotajwa kuwa na uwezekano mkubwa wa kupata mvua hizo ni Dar es Salaam, Tanga, Pwani (kikiwamo kisiwa cha Mafia), Zanzibar, Morogoro na Lindi.

"Uwezekano wa kutokea mvua hizo ni mkubwa lakini athari zake tunategemea kuwa za wastani kwa maeneo mengi yaliyotajwa," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

TMA imetaja athari zinazoweza kutokea kuwa ni maeneo ya makazi kuzungukwa na maji, kusimama kwa baadhi ya shughuri za kiuchumi na kijamii pamoja na ucheleweshwaji wa usafiri.

Mamlaka imewataka wananchi na sekta husika kuchukua tahadhari na kuzingatia utabiri huo walioutoa jana.

Tayari mvua za msimu imeanza kunyesha maeneo mbalimbali ya nchi na baadhi ya mikoa imeripotiwa mvua hiyo kuleta mdhara kwa jamii.

Mkoani Ruvuma katika Wilaya ya Namtumbo juzi kuliripotiwa nyumba 133 za kijiji cha Likuyesekamaganga kuezuliwa na mvua iliyoambatana na upepo na kusababisha familia hizo kukosa makazi.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Julius Ningu, alinukuliwa na Nipashe jana akisema mvua hiyo ilinyesha Novemba 30 kwa dakika 45 na kusababisha madhara hayo, yaliyogusa pia zahanati na shule ya msingi.

# Wabunge wanavyoathiriwa na vitendo vya ukatili wa kijinsia

**Na Romana Mallya**

WABUNGE wametoa shuhuda zao namna wanavyokumbana na vitendo vya ukatili wa kijinsia majimboni na kwenye mitandao ya kijamii.

Kutokana na hali hiyo, wameihamasisha jamii kuwa wakati wa kumaliza unyanyasaji huo ni sasa ili kujenga jamii mpya.

Waliotoa shuhuda ni mbunge wa viti maalumu kupitia Chama Cha Mapinduzi (NGO Tanzania Bara) na balozi wa Covid19 Tanzania, Neema Lugangira na mbunge wa viti maalumu mkoa wa Shinyanga, Salome Makamba.

Wakizungumza jana jijini Dar es Salaam katika mkutano wa kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia mahali pa kazi ulioandaliwa na Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF), walikiri kuwa ni waathirika wa matukio hayo.

Akitoa mchango wake katika eneo hilo, mbunge Neema alishauri wakati wanaangazia ukatili wa kijinsia kazini wakumbuke mambo manne ili kuijenga jamii isiyopitia ukatili.

"Kundi la kwanza wafanyakazi wetu wa majumbani, tuhakikishe na wenyewe hawapitii ukatili wa kijinsia, hawa tunawaacha kwa muda mrefu na watoto wetu.

"Kundi la pili ni wabunge wanawake nimewakumbusha wadau wa ukatili wa kijinsia wanapopaza sauti zao ya ukatili kazini wasisahau pia wabunge wanawake tunapitia ukatili maeneo yetu ya kazi, mikoa, majimbo na mikutano tunayoshiriki."

Neema alisema ukatili mwingine ambao wanaupitia wabunge wanawake ni kupitia mitandao ya kijamii na athari wanazopata ni kufifisha juhudi wanazozifanya na matokeo yake wanalazimika kutoka mitandaoni.

"Athari kubwa ni kufifisha juhudi zetu za kuhamaisha vijana wa kike na wanawake kuingia kwenye ulingo wa siasa na hatimaye kufikia 50/50," alisema.

Alimshukuru Spika wa Bunge, Job Ndugai, kwa kuridhia wabunge wanawake kuwa na kikundi vinara wa kupinga ukatili wa kijinsia kwa wanawake wanasiasa ambapo wameanza kupaza sauti suala la ukatili mitandaoni.

"Mitandaoni ukituma kitu, mapokeo yanakuwa tofauti kwa mbunge au mwanasiasa mwanamke kwa sababu mijadala kwenye mitandao haiendi na hoja bali inageuka inakuwa uanamke, utaona wanaandika angalia nywele zake, anafaa kuwa hiki au kile, lakini kwa mwanaume huwa tofauti," alisema.

Alisema kwa upande wa majimboni wao kama wabunge wa viti maalum wanafanya kazi kwenye majimbo yote mkoa hivyo matatizo yanakuja kwenye wabunge wa majimbo.

Kundi la tatu alilitaja ni wasisahau eneo la kunyonyesha mahali pa kazi kwa sababu miongozo ya serikali ipo wazi kila ofisi inatakiwa iwe na chumba maalum ili mama anayenyonyesha aweze kukitumia.

Mbunge Salome alisema wanawake wenye uwezo wa kukabiliana na matatizo hayo ni wachache.

"Naweza kusema mimi ni mmoja wapo pamoja na wimbi kubwa limepita hapa katikati la kushambulia wanawake kwa sababu yoyote nimeweza kuhimili, najaribu kufikitia kwa wanasiasa wachanga wanawezaje," alihoji.

Salome alisema imemchukua miaka mitano kujengwa bungeni mpaka sasa anaweza kujisimamia na kueleza kuwa kumrudisha nyuma ni kuwarudisha wanawake wengi wanaomtazama.

Aliwashukuru wadau wanaopinga ukatili wa kijinsia na kueleza kuwa anaamini baada ya mjadala wao watakuja na maazimio ambayo yatawezesha sheria zinasimamiwa na watu wanatetea haki zao.

Ofisa wa Tathmini na Ufuatiliaji kutoka WiLDAF, Rehema Maro, alisema wamekutana kufanya mjadala kuhusu ukatili wa kijinsia mahali pa kazi.

Alisema shirika hilo limekuwa likitengeneza mradi wa wanawake na ajira na wamefikia viwanda 100 na utafiti wa awali walibaini wanawake na vijana wanapitia matukio ya ukatili ukiwamo udhalilishaji wa kingono.

Alisema wakati wa utekelezaji wa mradi wamebaini ukatili mahali pa kazi unaathiri makundi hayo, familia, jamii na pia waajiri kwa sababu aliyefanyiwa uwezo wake wa kazi hupungua.

Alisema katika viwanda 100 katika utafiti wa awali waligundua asilimia 75 ya wanawake wanapitia vitendo vya udhalilishaji kingono kutoka kwa kiongozi kwenda kwa mwajiriwa.

Pia alisema walibaini ukatili huo hufanywa baina ya mfanyakazi na mfanyakazi.

"Elimu tunayotoa inaangalia ngazi mbili, ya mifumo na wafanyakazi wenyewe, tunafanya kazi karibu na TUICO (Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri) na ATE (Chama cha Waajiri Tanzania," alisema.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

MFUKO WA MISITU TANZANIA

Mfuko wa Misitu Tanzania

Kwa Kudumisha Ugharimiaji wa Usimamizi wa Misitu

## TANGAZO

### MABADILIKO YA UTARATIBU WA KUWASILISHA MAOMBI YA RUZUKU

Mfuko wa Misitu Tanzania unawajulisha wananchi kuhusu mabadiliko ya utaratibu wa kuwasilisha maandiko ya miradi kwa ajili ya kuomba ruzuku.

Kwa mujibu wa Kanuni za kusimamia utoaji ruzuku za mwaka 2021, maandiko ya miradi kwa ajili ya kuomba ruzuku yatapokelewa mara moja tu kwa mwaka badala ya mara tatu kwa mwaka kama ilivyokuwa hapo awali.

Tangazo la kuitisha maombi ya ruzuku litatolewa mwezi Desemba kila mwaka na mwisho wa kupokea maandiko ya miradi kwa ajili ya kuomba ruzuku utakuwa tarehe 31 Machi kila mwaka.

Tangazo la kuitisha maandiko ya miradi ya kuomba ruzuku kwa mwaka 2022 litatolewa mwezi Desemba, 2021 na mwisho wa kupokea maombi utakuwa tarehe 31 Machi 2022.

Wananchi wote wenye nia ya kuomba ruzuku inayotolewa na Mfuko wa Misitu Tanzania wanashauriwa kuzingatia ipasavyo maelekezo yaliyomo kwenye Tangazo la kuomba ruzuku litakalotolewa tarehe 15 Desemba, 2021.

Kwa ufafanuzi zaidi unaweza kuwasiliana na maafisa miradi wa Mfuko wa Misitu Tanzania kwa namba za simu **0754 651868 au 0652415692**

**Imetolewa na**
**Menejimenti ya Mfuko wa Misitu Tanzania.**

116598802

HABARI KITAIFA

# Bastola yatelekezwa chooni

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

WAKATI Jeshi la Polisi likifuatilia utekelezaji wa agizo la serikali kuwataka wote wanaomiliki silaha kinyume cha sheria kuzisalimisha, mkoani Morogoro bastola aina ya Browing imepatikana ikiwa imetelekezwa kwenye choo cha baa katika Kata ya Bigwa, Manispaa ya Morogoro.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Morogoro, Fortunatus Musilimu, alibainisha tukio hilo jana katika taarifa yake kwa waandishi wa habari kuhusu operesheni iliyofanyika kwa kipindi cha wiki tatu maeneo mbalimbali.

Kamanda Musilimu alisema bastola hiyo yenye namba CZ 92 CAI 35 na usajili TZ CAR 88604, ikiwa na risasi moja ndani ya magazine, ilipatikana ikiwa imetelekezwa ndani ya choo cha baa hiyo.

Alisema bastola hiyo ilitelekezwa Novemba 13 mwaka huu majira ya saa 2:30 usiku ndani ya choo cha baa hiyo.

"Tunaendelea kuwambia wanaomiliki silaha kinyume cha taratibu tunasisitiza kuzisalimisha silaha hizo na kutaendelea kuhamasisha jamii kwenye mikutano ikiwa ni utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi," alisema.

Kamanda Musilimu alisema kwa sasa bado wanaendelea na uchunguzi zaidi ili kumpata aliyetelekeza bastola hiyo.

Katika hatua nyingine, kiongozi huyo alibainisha kuwa operesheni yao hiyo imenasa watuhumuwa wa uhalifu 116. Kati yao, 32 wanadaiwa kujihusisha na matukio mbalimbali ya kihalifu na wote wamefikishwa mahakamani.

Alisema watuhumiwa 84 walikamatwa kwa makosa ya kuuza na kusafirisha dawa za kulevya aina ya bangi. Wakati huo, jumla ya ekari 70 za mashamba ya bangi yaliyokuwa yamelimwa na baadhi ya wananchi wa kitongoji cha Changa na Lugala, Kijiji cha Mnyanza, Kata ya Mzumbe wilayani Mvomero, yameteketezwa na jeshi hilo kwa kuchomwa moto.

Kamanda Muslimu alisema watuhumiwa wanne wanashikiliwa kwa kuhusishwa na kilimo hicho na upelelezi utakapokamilika watafikishwa mahakamani.

Kwa mujibu wa kamanda huyo ekari hizo zingeweza kuzalisha magunia 856 kwa wastani wa kila ekari moja kuvunwa magunia 15 ambayo yanakadiriwa kuwa na uzito wa kilo 21,396, sawa na tani 21 kwa makadirio ya uzito wa kilo 25 kwa kila gunia.



Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Ardhi (ARU), Prof. Evaristo Liwa (wa pili kushoto), akikabidhi zawadi kwa mwanafunzi mshindi wa jumla kwenye masomo ya mwaka 2020/21, Grace Mhina, wakati wa sherehe za utoaji wa zawadi kwa wanafunzi waliofanya vizuri katika chuo hicho, mkoani Dar es Salaam jana. Kushoto ni Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Taaluma), Prof. Gabriel Kassaga. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Zimamoto yaokoa kichanga aliyetupwa chooni

**Na Lilian Lugakingira, KARAGWE**

MTOTO mchanga, ameokolewa akiwa hai kutoka katika shimo la choo cha shule ya msingi Rukanyange wilayani Karagwe mkoani Kagera, baada ya kutupwa katika shimo hilo na mtu ambaye hajafahamika.

Kichanga huyo mwenye umri wa kati ya siku mbili hadi tatu, alikutwa akiwa amefungwa katika mfuko.

Kaimu Mkuu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani Kagera, Thomas Majuto, alisema kuwa tukio hilo lilitokea Jumatano, na kwamba walipata taarifa kuwa kuna sauti ya mtoto inasikika kutoka katika shimo la choo cha shule hiyo na kwenda kufanya maokozi.

"Askari wa Zimamoto walioko wilaya ya Karagwe waliwahi eneo la tukio, walipofika kweli walisikia sauti ya mtoto kutoka chooni, kazi ya kubomoa choo ilianza mara moja na walifanikiwa kumtoa mtoto huyo wa kiume akiwa hai," alisema Majuto.

Naye Mkuu wa Zimamoto wilaya ya Karagwe, Karata Ramadhan ambaye ndiye aliingia katika shimo la choo kumtoa mtoto huyo, alisema walishirikiana na askari wengine na wananchi kubomoa choo kisha yeye kuzama ndani na kumtoa.

"Baada ya kumtoa tulimpeleka na kumkabidhi Hospitali teule ya wilaya ya Karagwe ya Nyakahanga kwa lengo la kupimwa afya na kupewa huduma ya kwanza," alisema.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Nyakahanga, Dk. Furaha , alithibitisha kumpokea mtoto huyo akiwa hai, na kwamba baada ya kumpokea alihudumiwa na sasa hali yake inaendelea vizuri.

Kufuatia kuwapo kwa matukio ya mara kwa mara ya kutupa watoto chooni mkoani Kagera, baadhi ya wananchi akiwamo Mugisha Mathias waliishauri serikali kuwachukulia hatua watakaobainika kuhusika na matukio hayo, huku wakiwashauri wananchi kumrudia Mungu.

# Saba wahukumiwa kujipatia mamilioni kwa udanganyifu

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara imewahukumu watu saba kifungo cha miaka saba jela au kulipa faini Sh.300,000 kila mmoja kwa kosa la kuisababishia hasara serikali ya Sh.16,704,316.

Aidha, mahakama hiyo imemuachia huru mshtakiwa namba moja, Kelvin Milanzi baada ya kuonekana kuwa hana hatia.

Hukumu ya kesi hiyo namba ECC04/2020 iliyotolewa jana iliwakabili washtakiwa wanane ambao walikuwa wakikabiliwa na makosa 12, likiwemo la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Mwendesha mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wilaya ya Masasi, Charles Mtungila, alidai kuwa washtakiwa wa kesi hiyo walifunguliwa mashtaka Febuari 8, mwaka 2020, wakikabiliwa na makosa 12 likiwamo la kughushi, kosa la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kosa la kuisababishia hasara serikali ya Sh. 16,704,316

Washtakiwa hao kabla walikuwa Shamila Masali, Kevin Millanzi, Musa Mrope, Marry Milanzi, Faidha Anthony, Rashidi Mbwago, Prisca Mjunju na Yusta John wote wakazi wa wilaya ya Masasi.

Akitoa hukumu, Hakimu Batista Kashusha, alisema kutokana na mahakama kujiridhisha na ushahidi uliotolewa, mahakama hiyo inawahukumu washtakiwa hao saba kwenda jela miaka saba au kulipa faini ya Sh. 300,000 kila mmoja.

Alisema walitenda makosa hayo mwaka 2013 kwa nyakati tofauti kwa kughushi nyaraka za serikali na kulipwa fedha za fidia ya malipo ya mradi wa maji Masasi- Nachingwea (MANAWASA) Sh. 16,704,316 wakati hawakuwa wahusika ambao walipaswa kulipwa

Washtakiwa wote walishindwa kulipa faini, hivyo walipelekwa gerezani.

**HABARI KITAIFA**

## Jukwaa la biashara Italia, Tanzania lafana

**Na Mwandishi Wetu,** ROMA

JUKWAA la kwanza la biashara na uwekezaji kati ya Tanzania na Italia limefanyika jijini Roma kwa mafanikio makubwa, likiwakutanisha wafanyabiashara na wawekezaji zaidi ya 250 kutoka nchi zote mbili katika kipindi hiki cha UVIKO-19.

Pamoja na mambo mengine, jukwaa hilo limewawezesha wafanyabiashara na wawekezaji kujadili fursa, uwezekano wa ubia, changamoto zinazokabili mazingira ya biashara na njia ya kuboresha uhusiano wa kibiashara kati ya Tanzania na Italia ambapo limendaliwa na Ubalozi wa Tanzania nchini Italia kwa kushirikiana na Kituo cha Taifa cha Uwekezaji (TIC) na Mamlaka ya Taifa ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA).

Ujumbe wa Tanzania umeongozwa na Naibu Waziri wa Madini, Prof. Shukrani Manya, aliyewaeleza wawekezaji na wafanyabiashara kutoka Italia kuwa Tanzania kwa sasa imejikita kuwekeza katika miundombinu wezeshi ya uwekezaji.

Alisema kuwa Rais Samia Suluhu Hassan ameliweka suala la uwekezaji kama kipaumbele katika kuhakikisha wawekezaji kutoka nje na ndani ya nchi wanawekeza fedha na mitaji yao ili kukuza biashara na ajira kwa Watanzania na kuwezesha uchumi wa Tanzania kusonga mbele.

"Tanzania inathamini uwekezaji na sasa inapiga hatua kwa kuweka miundombinu wezeshi, pia Tanzania kama nchi tunamshukuru Mungu kwamba lengo la njozi yetu na maono yetu ya imeweza kufikia malengo yake miaka mitano kabla muda uliokuwa umepangwa.

"Lengo kubwa lilikuwa ni kuifanya Tanzania kwenda katika viwango vikubwa vya kiuchumi na mwaka 2020 Tanzania ilitangazwa na Benki ya Dunia kuingia katika Uchumi wa Kati," alisema Prof. Manya.

Aliongeza kuwa katika miaka mitano ijayo Tanzania inapoelekea kumaliza njozi yake, inatamani kuendelea kukuza uchumi na ikiwezekana ihame katika uchumi wa kati na kuhamia uchumi wa juu.

Alisema Tanzania inajivunia kuwa na hali ya amani na utulivu na katika nchi za ukanda wa maziwa makuu, ikijivunia kuwa na siasa safi yenye utulivu na amani ndani yake.

"Mfano tumeona mwekezaji aliyewekeza katika kilimo cha Pareto ameshuhudia kwa kusema kuwa Tanzania ni nchi ya amani na utlivu na kuwasihi Waitaliano kuja kuwekeza Tanzania," aliongeza Prof. Manya.

Balozi wa Tanzania Italia, Mahmoud Thabiti Kombo, alisema kufanyika kwa jukwaa la biashara na uwekezaji ni kuwavutia wafanyabiashara na wawekezaji wa sekta mbalimbali kutoka Italia kuwekeza zaidi Tanzania ili kukuza uchumi wa pande zote mbili.

# Maabara 114 zasitishiwa huduma

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

BODI ya Maabara Binafsi za Afya Tanzania imetoa ilani ya kusitisha huduma kwa muda kwa maabara 114 ili kupisha maboresho, baada ya kubaini mapungufu wakati wa ziara ya ukaguzi.

Aidha, ofisi ya msajili huyo imewafikisha katika kituo cha polisi cha wilaya ya Mvomero mkoani Morogoro kwa udanganyifu wa vipimo kwa wateja.

Sababu nyingine iliyosababisha kuwafikisha polisi wamiliki hao ni huduma za maabara kutolewa na mtu asiye mtaalamu wa maabara na hivyo kuhatarisha maisha ya watu wanaofika kufuata huduma katika maabara hizo.

Akizungumza jana jijini Dodoma 3,2021 Msajili wa Bodi hiyo, Dominic Fwiling'afu, alisema kuwa taratibu za kuwafikisha mahakamani wamiliki waliofikishwa katika kituo cha polisi cha Mvomero zinaendelea.

Alisema ukaguzi huo ulifanyika kati Aprili mwaka jana hadi Oktoba mwaka huu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) na Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi (PHAB).

Alifafanua zaidi ya kuwa ukaguzi huo umefanyika katika maabara 849 kwenye mikoa ya Arusha (107), Dar es Salaam (2,58), Mwanza (187), Tanga (44) na Morogoro (253).

"Kaguzi hizi zinaenda sambamba na utoaji wa elimu juu ya ubora wa huduma za maabara na kuwajengwea uwezo wataalamu wa maabara kwenye vituo vyao hivyo kila maabara ilipata fursa hii ya mafunzo,"alisema.

Aliongeza luwa tiba sahihi kwa mgonjwa hutegemea majibu sahihi ya vipimo vya maabara hivyo wamiliki na wataalamu wa maabara, waratibu wa huduma za maabara mikoa na halmashauri kote nchini washirikiane kuboresha huduma za maabara ili mgonjwa apate tiba sahihi.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akimsikiliza Mkurugenzi wa Shirika la Vijana (TAYOA), Peter Masika (kushoto), wakati alipotembelea banda la Shirika hilo wakati wa kilele cha maaadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani yaliyofanyika Kitaifa jijini Mbeya. Kulia ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), Jenister Mhagama. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mjane: H/shauri inataka kuninyang'anya viwanja

**Na Thobias Mwanakatwe**

MJANE, Hatra Tukale (66), mkazi wa mjini Tunduma wilayani Momba mkoani Songwe, amemuomba Rais Samia Suluhu Hassan aingilie kati haki itendeke akidai halmashauri ya mji wa Tunduma inataka kumnyang'anya viwanja vyake ambavyo aliuziwa na halmashauri hiyo mwaka 2007.

Akizungumza na waandishi wa habari, alidai aliuziwa viwanja hivyo ambavyo ni namba 183 na 184 kitalu 'A' mwaka 2007 na kupewa hati ya kuvimiliki 2011 ambapo tangu kipindi chote hadi mwaka huu, amekuwa akivilipia kodi kama sheria na taratibu zinavyoelekeza.

Tukale alidai baada ya kuuziwa viwanja hivyo na halmashauri na kukabidhiwa hati, alijitokeza mtu mmoja aliyefahamika kwa jina la Mohammed Sultan na kudai eneo hilo ni la kwake alilokuwa akilimiliki kiasili kabla ya halmashauri kutangaza kuyatwaa maeneo hayo.

Alisema kutokana na mgogoro huo alikubali kuyamaliza kwa kukubali kumlipa ili viwanja viendelee kubaki chini yake maana kosa lilifanywa na halmashauri ambayo ilimuuzia eneo hilo.

Mjane huyo huku akionyesha nyaraka mbalimbali, alisema suala hilo liliibuka tena baada ya Sultan kufariki dunia ambapo watoto wake walitaka wapewe eneo la baba yao na walikwenda mahakamani kudai haki yao.

Kwa mujibu wa nyaraka ambazo gazeti hili imeziona, mahakama iliamuru kuwa halmashauri ya Mji wa Tunduma ndiyo itoe fidia kwa Sultan kwa sababu haikufuata utaratibu wakati wa kulitwaa eneo hilo kabla ya kumuuzia mjane huyo.

Kufuatia uamuzi huo wa mahakama, mwaka 2017 halmashauri ilifanya tathmini ya viwanja hivyo na kubaini Sh. milioni 11 ndicho wanastahili kulipwa watoto wa Sultan, uamuzi ambao haujatekelezwa hadi sasa ikiwa ni miaka minne tangu uamuzi wa mahakama utolewe.

Alidai kuwa wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu 2020 aliandika bango na kwenda nalo kwenye mkutano wa kampeni uliokuwa ukihutubiwa na aliyekuwa Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, kipindi hicho, lakini kabla hajafika nalo eneo la tukio alinyang'anywa na maofisa halmashauri ambao walimuomba na kumwahidi kulishughulikia tatizo lake.

Tukale alisema baadaye Mkurugenzi wa Mji wa Tunduma kipindi hicho, Castory Sigala, alimwandikia barua yenye kumbu namba TTC/20/15/85 ya Agosti 14, 2018 na kumjulisha kuwa hawawezi kumlipa mmiliki wa asili na badala yake yeye (Tukale) watampa viwanja vingine tofauti na vile alivyouziwa na halmashauri.

"Nilikwenda halmashauri nikapelekwa kuonyeshwa viwanja vingine ambavyo ni namba 233 na 234 kitalu J vilivyopo eneo la Chapwa Tunduma, lakini sikuvipenda nikawaeleza bora nibaki kwenye viwanja vyangu vya awali walivyouziwa wao halmashauri," alidai. Alisema alianza kuviendeleza viwanja vyake vya awali kwa kujenga jengo na kuchimba kisima, lakini katika hali ya kushangaza halmashauri ilivunja jengo alilokuwa amejenga na kufukia kisima kilichokuwa kimechimbwa.

Alisema kufuatia tukio hilo, aliamua kwenda Dodoma kufuatilia ambapo alionana na mbunge wake David Silinde (Mbunge wa Tunduma), ambaye alimuunganisha kwa viongozi wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Akiwa wizarani hapo aliunganishwa na Katibu Mkuu wa Wizara ambaye alimpigia simu Kamishna wa Ardhi Mkoa wa Songwe alishughulikie suala la mjane huyo ambaye alikubali kufanya hivyo na kumwahidi siku ya kufika ofisini kwake kulitafutia ufumbuzi suala hilo.

Hata hivyo, alidai baada ya kurejea Songwe wiki tatu zimepita kwa ajili ya kuonana na Kamishna wa Ardhi Mkoa wa Songwe, na kwamba kila akimpigia simu hapokei, hivyo amekata tamaa.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Tunduma, Philemon Magesa, alipoulizwa alisema anaufahamu mgogoro huo, lakini hawezi kuzungumzia kwa undani kwa sababu yeye bado ni mgeni na kumwelekeza mwandishi kumfuata Mkuu wa Idara ya Ardhi na Mipango miji ndiye alitole ufafanuzi.

Mkuu wa Idara ya Ardhi na Mipango Miji, Abdul Mbwana, alipoulizwa alikiri halmashauri kufanya makosa katika suala hilo na kwamba kilichokwamisha ni kushindwa kumlipa fidia mmiliki wa asili (Sultan) tangu mwaka 2017 tathmini ni ukosefu wa fedha.

## MAONI & UCHAMBUZI

**Nipashe**
MWANGA WA JAMII

# *Hongera Tembo Warriors, Mungu ibariki Tanzanite*

**WAKATI** Timu ya Soka ya Taifa ya Watu Wenye Ulemavu (Tembo Warriors), ikiandika historia ya kufuzu tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia za mashindano hayo kwa mara ya kwanza, mabinti wa Kitanzania wenye umri chini ya miaka 20 (Tanzanite Queens), nao watashuka dimbani kuvaana na wenzao kutoka Burundi.

Tembo Warriors ilipata tiketi hiyo baada ya kuichapa Cameroon mabao 5-0 kwenye mchezo wa hatua ya robo fainali ya michuano ya Afrika (CANAF), iliyofanyika hapa nchini, ingawa imeshindwa kutinga fainali kufuatia kupoteza mechi iliyofuata.

Tunapenda kuchukua nafasi ya kipekee kuipongeza Tembo Warriors kwa mafanikio ambayo wamefikia kwenye michuano hiyo, na kwa kufanya hivyo watambue wamelipa heshima jina la Tanzania.

Kama ilivyo kwa timu nyingine, Tembo Warriors walikuwa na changamoto mbalimbali, lakini wachezaji wake waliamua kujituma na kuweka mbele maslahi ya taifa.

Kwa kuamini wameingia katika michuano hiyo wanapeperusha bendera ya Tanzania, wanastahili kupewa pongezi na ikiwezekana hata kutunukiwa zawadi mbalimbali kama 'maaskari' wengine walivyopewa ili kuendelea kuwajenga na kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kujiandaa na mashindano ya dunia.

Pongezi za Tembo Warriors, haziwezi kukamilika bila kumtaja Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, ambaye aliikabidhi timu hiyo kiasi cha Sh. milioni 150 ili ziwasaidie kwenye maandalizi na gharama za kila siku wakati wote wa mashindano.

Motisha hiyo ya Rais Samia ilikuwa na maana kubwa kwa timu hiyo, na kwa kufahamu umuhimu wake, Tembo Warriors walienda kutekeleza kile kilichotarajiwa na Watanzania hasa ukizingatia fainali hizo za CANAF zimefanyika kwenye ardhi ya Tanzania.

Katika hali halisi, sasa Tembo Warriors inahitaji zaidi misaada ya fedha za vifaa kwa ajili ya kufanya maandalizi ambayo yataendana na ukubwa wa mashindano yaliyoko mbele yao.

Rais Samia alifungua njia, huu ni wakati mwingine kwa makampuni, taasisi na wadau wa michezo kuidhamini timu hiyo ili iweze kwenda Uturuki kushindana na si kushiriki.

Ni imani yetu kuwa timu hiyo ikiwa imara, basi itakuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kupata matokeo chanya, na hayo yote hayawezi kufanyika bila ya misaada kutoka kwa wadhamini mbalimbali.

Kwa upande wa Tanzanite, leo mchana inashuka dimbani kuwakaribisha wapinzani wao kutoka Burundi katika mchezo wa kwanza wa raundi ya pili kwenye michuano ya kusaka tiketi ya kwenda Costa Rica katika fainali za Dunia zitakazochezwa mwakani.

Huu ni wakati mwingine wa Watanzania kuiombea dua Tanzanite Queens ifanye vyema katika mechi hiyo na baadaye ya marudiano itakayochezwa ugenini Bujumbura ili itimize ndoto za kushiriki fainali hizo kwa mara ya kwanza.

Tanzanite Queens ambayo ilianza kampeni hiyo kwa kuwaondoa Eritrea, inahitaji kupata ushindi mnono ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kusonga mbele itakaposafiri kwenda Bujumbura kumalizia dakika 90 zilizobakia.


Tukumbuke kuitakia mema Tanzanite, sio tu kutawapa sifa wachezaji, lakini nchi itaendelea kupata heshima katika ngazi ya kimataifa.

Tunawakumbusha wachezaji kuendelea kujituma kwa sababu michuano hiyo ni nafasi nyingine ya kutangaza vipaji vyenu na kwa wale watakaong'ara watakuwa wamejitengenezea 'daraja' la kwenda kucheza soka la kulipwa huko ughaibuni.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# *Fahali wawili hawakai zizi moja*

Na Barnabas Maro

**FAHALI** wawili hawawezi kukaa zizi moja kwa sababu kila mmoja atataka awe mkuu wa zizi, hivyo watashinda kutwa wakipigana.

Fahali ni dume la mnyama mkubwa kama vile nyati au ng'ombe (enye nguvu na ujasiri.) Ndivyo zilivyo timu za Simba na Yanga zilizo na makao yao jijini Dar es Salaam.

Uungwana ni hali ya mtu kuwa tayari kumfanyia mtu mwingine wema na insafu; utu. Hali ya kustaarabika au kuwa muungwana; ustaarabu hali ya kuwa mtu huru.

Ilivyo sasa humu nchini, Simba na Yanga hazina uungwana, hasa mashabiki yaani watu wenye mapenzi, hamasa kubwa juu ya jambo au kitu fulani ambao wengi wao sio wanachama wa timu hizo bali ni mashabiki tu.

Sasa hata baadhi ya viongozi wa klabu hizo wameingia kwenye upuuzi huo wakiwamo baadhi ya waandishi wa habari za michezo.

Sasa soma jinsi waandishi wanavyozidi kuzifanya Simba na Yanga zizidi kuwekeana mafundo yaani chuki ambayo mtu huiweka moyoni dhidi ya mtu ambaye amemtendea vibaya; kinyongo. Zamani, Yanga na Simba zilikuwa moja na baadaye zikatengana. Tangu wakati ule zimekuwa maadui na sio 'watani wa jadi' kama inavyosemwa kwani watani hawadhuriani bali husaidiana.

Sasa timu hizo zimekuwa zikirushiana vijembe (tamathali ya semi ambayo hutumika kwa madhumuni ya kumsema mtu kwa njia ya upambaji.)

**"Inyeshe mvua, liwake jua... Simba baba lao..." "Mwe... watakuja kweli!" Simba waapa: "Watajua hawajui." "Kwani sisi na wao lini?" "Tukutane Desemba 11 Tumalizane." "Nina Sapraizi yao." "Mtaniee, Utajua hujui."**

Kama unasoma safu hii ya "Muungwana Lazima Nilonge," soma yafuatayo yaliyoandikwa kwenye gazeti fulani maarufu humu nchini;

"Inyeshe mvua, liwake jua... Simba baba lao..." "Mwe... watakuja kweli!" Simba waapa: "Watajua hawajui." "Kwani sisi na wao lini?" "Tukutane Desemba 11 Tumalizane." "Nina Sapraizi yao." "Mtaniee, Utajua hujui."

Hizi ni baadhi ya tambo na usemaji wa timu hizo. Kwenye mkutano wa Simba uliofanyika Novemba 21, mwaka huu viongozi kadhaa wa klabu hiyo waliipiga Yanga vijembe vya aina mbalimbali huku wanachama wakishangilia sana.

Jambo lingine la kushangaza ni jinsi baadhi ya wananchi wetu wanavyoonyesha ujinga wao kwa ama kutokwenda viwanjani pale timu zetu za taifa zinapopambana na za ughaibuni (nchi zilizo mbali na nchi yetu) kumbe tunajifedhehesha wenyewe!

Hivi karibuni, timu ya watu wenye ulemavu nchini Tanzania inayoitwa Tembo Warriors waliichabanga Cameroon mabao 5-0 na hivyo kufanikiwa kukata tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Dunia zitakazochezwa Uturuki hapo mwakani.

Hata hivyo waliokuwa uwanjani kushangilia ilisikitisha na kushangaza kutokana na idadi ndogo sana ya walioingia kuwaunga mkono wawakilishi hao wa nchi. Ni aibu na fedheha, yaani nazaa, izara kwa Watanzania! Tujirekebishe jamani.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

# Bil. 1/- kupanga maeneo Rorya

**Na Munir Shemweta**

SERIKALI imeipatia halmashauri ya wilaya ya Rorya mkoa wa Mara Sh, bilioni moja kwa ajili ya mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK) katika wilaya hiyo na kipaumbele kikubwa ni eneo la mkakati la mji wa Kirongwe uliopo mpaka wa Tanzania na Kenya.

Hayo yalibainishwa jana na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, alipokuwa akizungumza na wakazi wa kijiji cha Kirongwe kata ya Bukura wilayani Rorya mkoa wa Mara akiwa katika zira ya siku moja mkoani humo.

Mabula alisisitiza kuwa wakati wa kuupanga upya mji huo wa Kirongwe kupitia mradi wa KKK hakuna eneo la mwananchi litakalochukuliwa bila ya kulipwa fidia.

"Serikali imetoa shilingi bilioni moja kama mkopo kwa ajili ya upangaji maeneo mbalimbali wilayani Rorya ikiwamo kuupanga vizuri mji wa Kirongwe uliopo mpakani mwa Tanzania na Kenya na lazima fidia ilipwe kabla ya kuchukua maeneo ya wananchi " alisema Dk. Mabula.

Kwa mujibu wa Mabula, kupitia mradi huo mji wa Kirongwe utapangwa vizuri na kuainishwa maeneo ya makazi, uwekezaji, viwanda pamoja na huduma za jamii na kusisitiza kuwa upangaji huo ni vyema ukazingatia pia makundi maalumu kama vile wamachinga na mamalishe.

Mkuu wa Idara ya Ardhi halmashauri ya wilaya ya Rorya, Fredy Kyalawa, alieleza kuwa fedha walizopatiwa halmashauri ambazo ni za mkopo zitatumika kupanga maeneo katika wilaya ya Rorya na kipaumbele ni eneo la mpaka wa Tanzania na Kenya katika mji wa Kirongwe.

"Fedha tuliyopewa tutaitumia kupanga na kupima maeneo mbalimbali katika wilaya yetu ya Rorya na kipaumbele ni eneo la mkakati la mji wa Kirongwe ambapo huko tutalipa fidia na kufanya urasimishaji makazi holela kwa takriban viwanja 5,000 na baada ya hapo tutaenda maeneo mengine kama Shirati, Utegi, Mika na Kinesi," alisema Kyalawa.

Wananchi wa Kirongwe kupitia mkutano na Mabula walieleza kuwa pamoja na mpango wa upangaji upya mji huo, kuna hatari wakazi hao kuwa watazamaji kwa fursa zitakazokuja kutokana na changamoto kadhaa wanazopata ikiwemo ile wanayopata wakati wa kufanya shughuli zao za uvuvi.

"Tunashukuru kwa serikali kuamua kuendeleza mji wetu wa Kirongwe ila kuna hatari ya sisi kuwa watazamaji maana hivi sasa hatuna amani katika eneo la ziwa, Wakenya wanasema wamenunua ziwa tunaomba kilio chetu ukipeleke kwa Rais Samia," alisema Samson Sabanya.

# NEC yaanza kupokea, kuapisha mawakala uchaguzi Ngorongoro

**Thobias Mwanakatwe**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) itaanza kupokea, kuwatambulisha na kuwaapisha mawakala wa wagombea wa vyama 11 wanaowania ubunge katika uchaguzi mdogo jimbo la Ngorongoro mkoani Arusha.

Msimamizi Mkuu wa uchaguzi katika jimbo hilo, Dk. Juma Mhina, akizungumza na gazeti hili jana, alisema leo itafanyika semina ya kutoa maelekezo na kuwaapisha mawakala wa vyama vyote.

Kuhusu mwenendo wa kampeni, alisema vyama vyote vimeshafanya uzinduzi wa kampeni kulingana na ratiba iliyopo, na kwamba hakuna malalamiko yeyote yaliyotolewa na chama chochote.

"Tangu kampeni zimeanza Novemba 16, mwaka huu, wagombea wa vyama vyote wanafanya kampeni kama kawaida na hakuna chama ambacho mgombea wake amekwama kufanya kampeni kutokana na sababu zozote zile," alisema. Hivi karibuni NEC ilitangaza kuwa imetenga vituo 310 kwa ajili ya zoezi la kupigia kura katika uchaguzi huo ambao watu 115,858 wamejiandikisha kwa ajili ya kupiga kura.

Wagombea na vyama vyao ambao wanachuana katika kinyang'anyiro hicho ni Emmanuel Lekishoni Shangai (CCM), Simon Jonhson Bayo (SAU), Amina Amiri Mcheka (NLD), Mary Moses Daudi (UPDP) na Frida Marko Nnko (UMD).

Wengine ni Paulo Mwita Makuru (UDP), Shafii Kitundu (ADC), Feruziy Feruziyson (NRA), Simon P Ngilisho (Demokrasia Makini), Jonson Gagu (ACT-Wazalendo) na Zuberi Hamis (ADA TADEA).

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na NEC ni kwamba kampeni kwa ajili ya uchaguzi huo zilianza tangu Novemba 16, na zitahitimishwa Desemba 10 na siku ya kupiga kura itakuwa ni Desemba 11, mwaka huu.




Ofisa Mshauri Mwandamizi wa Taasisi ya, EngenderHeath, Dk. Katanta Simwanza, akitoa mada wakati wa Kongamano la siku 16 la kupinga ukatili wa Kijinsia lililofanyika jijini Dar es Salaam jana liliandaliwa na Taasisi ya kutetea unyanyasaji wa Kijinsia Wildaf. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Serikali yaikosha SUA utoaji fedha za ruzuku kwa wakati

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

CHUO Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimeishukuru Serikali kwa kukipatia kwa wakati fedha za ruzuku na maendeleo, na kwamba bila fedha hizo kisingeweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Kauli hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa Baraza la SUA, Jaji Mkuu mstaafu, Mohammed Othman Chande, katika kampasi kuu ya Edward Moringe, mjini Morogoro mbele ya Mkuu wa chuo hicho, Jaji mstaafu Joseph Warioba.

Alisema Serikali ilitoa ruzuku na fedha za maendeleo kwa wakati katika chuo hicho ambazo zimechangia kuwezesha ujenzi na uboreshaji wa miundombinu yake.

Alisema ,baraza lake limejipanga kutekeleza vyema majukumu yake kwa kuidhinisha mpango mkakati wa miaka mitano kuanzia 2021 hadi 2026, kusimamia utunzaji wa mali za chuo utekelezaji wa miradi ya maendeleo ukiwamo usimamizi wa mapato na matumizi ya fedha za chuo.

"Jaji Mkuu mstaafu Chande kwa kipindi cha miaka mitano baraza limetekeleza mambo mbalimbali ikiwamo kusimamia uanzishwaji wa Ndaki ya Mizengo Pinda na kusimamia matumizi ya mpango mkakati wa chuo".

"Nimshukuru kwanza kabisa na kipekee mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, Rais kwa kukuteua (jaji Warioba) tena kuendelea kuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwa kipindi kingine cha miaka mitano" alisema Jaji Mkuu mstaafu Chande.

Pia alimpongeza Jaji Warioba kutokana na rekodi yake nzuri ya utendaji kazi katika nyadhifa mbalimbali za juu ndani na nje ya nchi.

Alisema , Chuo Kikuu hicho kimeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi katika kuendeleza ubora katika mafunzo, utafiti, shughuli za ugani, huduma za jamii na uzalishaji mali ili kukabili na kutatua matatizo ya kilimo cha Tanzania na maisha ya vijijini.

"Majukumu hayo yanatimiza kikamilifu agizo la baba yetu wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambaye katika hotuba yake ya uzinduzi wa Chuo Kikuu hiki mwaka 1984, alisema namnukuu " Chuo Kikuu hiki lazima kitambue mahitaji ya kutatua mahitaji ya kilimo cha Tanzania na maisha huko vijijini."

Naye Makamu Mkuu wa SUA, Prof. Raphael Chibunda, aliishukuru Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kutenga Sh. bilion 74.2 kwa chuo hicho ambazo zitatumika kujenga majengo mapya na kuboresha miundo mbinu ya chuo.

Mlau wa mahafali ya 38 ya SUA kutoka Idara ya mimea vipando na kilimo cha bustani, Prof. Kalunde Sibuga, aliwashauri wahitimu kudhihirisha elimu waliyoipata kwa utendaji bora wa shughuli zao kwa umahiri na uaminifu ili kujiletea maendeleo binafsi na Taifa katika kutekeleza dhana ya uchumi wa viwanda.

Prof. Sibuga aliwaomba wahitimu hao kuitumia elimu na maarifa kujiletea maendeleo binafsi katika kuanzisha viwanda, kuendesha viwanda au kuendesha shughuli yoyote ambayo itakuwa mbele yao, huku wakizingatia maadili ya kazi.

# Jafo ataka nguvu zaidi mabadiliko ya tabianchi

**Na Mwandishi Wetu,** MUSOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, ameitaka jamii kuungana na serikali kwa kushiriki kikamilifu katika shughuli za kuhifadhi mazingira ikiwamo upandaji miti.

Jafo alitoa rai hiyo jana alipofungua Maonyesho ya Sita ya Kilimo Mseto katika viwanja vya Bweri Manispaa ya Musoma mkoani Mara, yaliyoandaliwa na shirika la Vi Agroforestry.

Alisema ni vyema kila kijiji kuanzia ngazi ya kaya kikawa na utamaduni wa kupanda miti na kuitunza, hatua itakayosaidia katika mapambano dhidi ya ukame na mabadiliko ya tabianchi kwa ujumla.

Akizungumza na wananchi waliokusanyika katika maonyesho hayo, Jafo aliwapongeza wadau hao wa maendeleo na kuwataka wananchi waunge mkono juhudi za serikali katika miradi mbalimbali inayotekelezwa ili kunusuru uharibifu wa mazingira.

"Kuna maeneo ya uwekezaji hasa hoteli zilizoko kando ya maziwa hayakaliki kwa sababu kiwango cha maji kimeongezeka, visiwa fungu kule Rufiji, Pwani vimemezwa na maji, vimepotea, maeneo mengine ukame umeshamiri na maeneo mengine kukosa maji.

"Tusipochukua hatua dunia itakuwa si sehemu salama ya kuishi ndugu zangu, tuna kazi kubwa ya kufanya ili kupambana na mabadiliko ya tabianchi," Jafo alitoa tahadhari.

Alisisitiza kuwa ni vigumu kupata mabadiliko katika nchi bila kuwekeza katika rasilimali watu ili wapate ufahamu wa kutosha wa kutafsiri mambo kinadharia na kivitendo hususan katika masuala ya mazingira na hivyo kuisaidia jamii.

Awali Mkuu wa mkoa wa Mara, Ally Hapi alisema mkoa umejipanga kuzindua kampeni ya upandaji miti katika maeneo mbalimbali yakiwamo makazi, taasisi na vijijini.

Hapi aliongeza kuwa kupitia kampeni hiyo watahamasisha wananchi kupanda misitu kwa ajili ya matumizi ya kuni badala ya kukata miti ovyo, hali inayosababisha uharibifu wa mazingira.

"Mheshimiwa waziri tumejipanga kupanda miti kwa wingi katika mkoa wetu kupitia kampeni hii ili tuweze kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi, kupata hewa safi na kuondosha hewa ya ukaa," alisema Hapi.

Mkurugenzi wa Shirika la Vi Agroforestry, Eva Aberg, alisema shirika hilo linathamini mchango wa wakulima wadogo, akitoa wito kwa watafiti na viwanda kufanya nao kazi bega kwa bega kupitia malighafi wanazozalisha.

Aberg alisema shirika hilo limeendelea kufanya kazi ya kutoa elimu kwa wakulima husasan katika mbinu za kilimo mseto ambacho hakiathiri mazingira ya mwanadamu.

Aliongeza kuwa kwa miaka mingi mabadiliko ya tabianchi yameleta athari kubwa kwa jamii nyingi duniani na kuwasababishia madhara hivyo alisisitiza juhudi za pamoja katika kuyakabili.

Maonyesho hayo hufanyika kila mwaka yakihusisha wakulima wa mazao tofauti kutoka mikoa mbalimbali nchini na kwa mwaka huu yanashirikisha washiriki kutoka Rwanda, Kenya, Uganda na mwenyeji Tanzania.




Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya NICOL Investment PLC, Erasto Ngamilaga (kushoto), akizungumza kwenye mkutano wa saba wa mwaka wa kampuni hiyo, jijini Dar es Salaam jana. Wa pili kushoto ni Mkurugenzi wa Kampuni hiyo, Mhandisi Peter Chisawilo, Katibu wa Kampuni, Benjamin Mwakagamba na Mwenyekiti wa Bodi, Dk. Gideon Kaunda. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Vodacom Tanzania yaoanisha mikakati ya maendeleo na serikali

**Na Elizabeth Zaya**

KAMPUNI ya Vodacom Tanzania imeweka mpango wa maendeleo na serikali kwa mwaka 2030.

Katika kutimiza mpango huo,imehakikisha kuwa na malengo ya maisha bora, jamii iliyoelimika, uchumi wenye ushindani kwa ukuaji endelevu wenye manufaa kwa wote, amani na utulivu na utawala bora.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa Masoko wa M-Pesa, Noel Mazoya, alisema Vodacom imejiwekea mikakati ya maendeleo ili kutimiza dhamira ya serikali ya kuunganisha sekta mbalimbali kwenye mfumo wa TEHEMA nchini na kujenga stadi na uwezo wa TEHEMA, utawala wa kidigitali na kutoa huduma za jamii kidigitali.

Vodacom Tanzania ina wateja zaidi ya milioni 15 katika soko la mawasiliano, huku ikitekeleza muongozo wa mkataba wake wa kijamii.

"Tumejiwekea lengo la kuunganisha asilimia 65 ya wananchi kwenye mtandao wa kasi ya broadband ifikapo mwisho wa mwaka 2021 na idadi ya asilimia 90 kabla ya mwaka 2024, lengo linalozidi lengo la serikali kwa asilimia 10. Kwa sasa uunganishwaji wa mtandao wa broadband unaotolewa na Vodacom unawafikia takribani asilimia 52 ya wananchi wanaoishi katika vijiji 1,184.

"Vile vile, kwa ushirikiano na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), Vodacom imepanua mtandao wake kuwafikia asilimia 92 ya wananchi, hivyo kuwa na mtandao mpana zaidi wenye ubora mkubwa zaidi wa huduma za sauti na data pamoja na huduma za kifedha na kijamii," aliongeza Mazoya.

Alisema teknolojia na mawasiliano vina uwezo kujenga jamii ya kidijitali yenye haki na jumuishi zaidi, na kwamba upatikanaji wa intaneti unawezesha ushiriki na ushirikishwaji kifedha.

Alibainisha kuwa baada ya mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19, mtandao wao ulihakikisha kuwa shughuli zao za kijamii na kiuchumi ziliendelea bila pingamizi, na kwamba watu wengi walianza kufanyia kazi majumbani ili kudhibiti usambaaji wa COVID.

"Kufanyia kazi nyumbani ilikuwa bora kuliko hata nilivyotegemea kwa mtandao bora wa 4G wa Vodacom," alifafanua Mazoya.

## Kampuni yaguswa utendaji wa NIT

**Na Mary Geofrey**

KAMPUNI ya Simba Supply Chain Solutions imekipongeza Chuo cha Usafirishaji cha Taifa (NIT) kwa kuzalisha wataalamu katika kada mbalimbali hasa katika kipindi ambacho nchi imejikita katika kuendeleza viwanda na kujenga uchumi imara.

Vilevile, uongozi wa kampuni hiyo umesema kwa kipindi kirefu umekuwa ukinufaika na mazao mbalimbali yanayozalishwa NIT katika kupata waajiriwa wenye sifa na kupata mafunzo mbalimbali kutoka kwa watendaji wao katika ngazi mbalimbali.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Hussein Dewji, alitoa pongezi hizo jana mkoani Dar es Salaam muda mfupi baada ya kutia saini makubaliano ya kushirikiana na NIT katika kuwapa zawadi wanafunzi wanaofanya vizuri katika masomo yao, kuajiri wahitimu na kuwapa nafasi ya kujifunza kwa vitendo.

Alisema wameamua kuingia makubaliano hayo na NIT kwa kuzingatia kuwa kampuni ina zaidi ya wafanyakazi 300 huku asilimia 60 wakiwa ni madereva ambao ni zao la NIT.

"Kutokana na unasaba huo, leo (jana) kampuni yetu imeingia makubaliano ya ushirikiano katika maeneo mbalimbali ikiwamo tafiti, mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi na mafunzo ya uwezeshaji kwa watendaji.

"Ushirikiano huu unalenga kuziba pengo la ujuzi katika mtiririko mzima wa thamani katika sekta ya usafirishaji na kutengeneza msingi wa maendeleo ya wafanyakazi ili kufikia uboreshaji endelevu, kuongeza tija na ufanisi katika kazi na mifumo na baadae kuongeza vipato vya taasisi zetu na nchi kwa ujumla," alisema Dewji.

Alisema kuwa kuanzia mwaka huu, kampuni hiyo itakuwa inatoa zawadi kwa wahitimu bora watano wa stashahada na shahada katika programu za uhandisi wa magari, usafirishaji na udereva wa kozi za muda mrefu wa magari ya mizigo.

Dewji aliahidi kuwa kampuni hiyo itaendelea kuwekeza katika nyanja mbalimbali na kutoa fursa kwa Watanzania wote.



# Maduka ya nyama nchini yahadharishwa kuhusu dawa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAMILIKI wa maduka ya kuuza nyama nchini wametahadharishwa kuhusu matumizi ya dawa za kuua wadudu kwenye maduka yao yakiwa na bidhaa hiyo kwa kuwa ni moja kati ya sababu kuu ya ugonjwa wa saratani kwa watumiaji wa kitoweo hicho.

Aidha, wananchi wametakiwa kuacha kununua nyama kwenye maduka yaliyopulizwa dawa za kuua wadudu, huku bidhaa hiyo ikiwa ndani ili kuepuka magonjwa hayo.

Msajili wa Bodi ya Nyama Tanzania, Dk. Daniel Mushi, alitoa tahadhari hiyo wakati wa mkutano wake na waandishi wa habari uliofanyika jijini hapa jana.

Mushi, aliwataka wamiliki wa maduka ya kuuza nyama nchini kuacha tabia ya matumizi ya dawa za kuua wadudu kwa sababu yanasababisha magonjwa mbalimbali.

"Matumizi ya dawa hizo za kuua wadudu kwenye maduka ya nyama ni hatari kwa afya ya mlaji kwani zinaweza kusababisha maradhi mbalimbali ikiwemo saratani," alisema.

Alisema kuwa bodi hiyo inatoa katazo kwa wafanyabiashara wa maduka ya nyama kuacha matumizi ya kuua wadudu kwenye maduka hayo yakiwa na nyama ndani ili kuepuka magonjwa hayo.

Alibanisha kuwa wanachotakiwa kufanya ni usafi kabla ya kuingiza nyama na baada ya kufungakazi sio kupulizia hizo dawa za kuua wadudu.

Alisema wadudu hao wamekuwa wakivutiwa na harufu mbaya inayotokana na kuharibika kwa nyama kwenye maduka hayo kwa sababu hayafanyiwi usafi.

Kadhalika, aliwashauri kuhifadhi nyama kwenye majokofu kuepuka kuwavutia wadudu wanaopenda uchafu kama inzi au kununua nyama kulingana na hitaji la wateja wake.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara hao kutumia misumeno wakati wa kukata nyama na kuepuka kutumia magogo kwa sababu yanahifadhi uchafu.

Pia, aliwataka kuweka chanzo cha maji ya moto kwenye maduka yao kwa ajili ya kusafisha vifaa vya kukata nyama pamoja na kuweka viyoyozi kupunguza kasi ya kuharibika kwa nyama.

Aliongeza kuwa nyama isafirishwe kwa kutumia magari maalumu ya kubebea ili kuzuia uharifu wa kitoweo hicho na wafanyabiashara hao kununua nyama kwenye machinjio iliyosajiliwa na bodi hiyo.



Msajili wa Bodi ya Nyama Tanzania, Dk. Daniel Mushi akionyesha kwa waandishi wa habari, jijini Dodoma juzi, dawa za kuua wadudu zinazotumiwa na baadhi ya wafanyabiasha kunyunyiza kwenye maduka ya kuuza nyama ili kuua wadudu mbalimbali, kitendo kinachohatarisha afya ya watumiaji wa kitoweo hicho. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# DC awapa angalizo wadau miradi ya Ukimwi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, amewaonya wadau wanaotekeleza miradi ya mapambano dhidi ya Ukimwi kutoitumia kuwa sehemu ya kujinufaisha wao binafsi.

Aidha, Shekimweri, amewaambia kuwa badala ya kujinufaisha wao binafsi, miradi hiyo itumike kwa ajili ya malengo ya kuwawezesha watu walioambukizwa Virusi Vya Ukimwi (VVU) waweze kujikimu katika mahitaji mbalimbali.

Onyo, hilo la mkuu wa wilaya alilitoa juzi wakati alipokuwa akizungumza na wananchi kwenye maadhimisho ya siku ya ukimwi duniani yaliyofanyika kiwilaya kata ya Nzunguni jijini Dodoma.

Alisema baadhi ya wadau wanaojihusisha na mapambano dhidi ya maambukizi ya Ukimwi,miradi yao inaishia kwenye matumbo yao badala ya walengwa kama walivyoomba kwa wafadhili wao.

Alisema kwa upande wa serikali haitakubali kukaa kimya dhidi ya wadau hao ambao wamekuwa wakitumia nafasi hiyo kwa ajili ya kujinufaisha wao binafsi.

"Hapa napenda nitoe wito kwenu nyinyi halmashauri ya jiji, mratibu wadau wote ili muweze kujua kazi zao za mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU au fedha zao zinafanya kazi kama walivyoomba na kubaini kama zinaishia kwenye mambo yao binafsi," alisisitiza.

Alisema kuwa siyo vizuri kuona ama kusikia kuwa tatizo la Ukimwi bado linaongezeka wakati kuna wadau wanaopatiwa mamilioni ya fedha kwa ajili ya kupambana, lakini walengwa hawafikiwi.

Akizungumza kwenye maadhimisho hayo Mwenyekiti wa kamati ya Ukimwi wilaya, Naibu Meya wa Jiji la Dodoma, Emmanuel Chibago, alisema kuwa halmashauri hiyo itahakikisha wadau wote wanaojihusisha na mapambano hayo wanaratibiwa na kazi zao zinawafikia wahusika.

Hata hivyo, Chibago aliwataka watu kuwa na tabia ya kupenda kupima afya zao ili waweze kujitambua kama wapo salama kiafya.

# BAKWATA yaagiza ukaguzi wa madrasa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

BARAZA Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) wilaya ya Dodoma Mjini limeagiza kufanyika kwa ukaguzi wa kina katika majengo ya madrasa na mabweni ya wanafunzi kuhakikisha miundombinu yake inakuwa kwenye mazingira salama na safi.

Aidha, ukaguzi huo utaepusha uwezekano mkubwa wa mlipuko wa magonjwa hususan katika kipindi hiki cha mvua.

Agizo hilo lilitolewa na Mwenyekiti wa Baraza hilo, Bashiru Omary wakati wa ziara yake ya kukagua majengo hayo yanayomilikiwa na Bakwata.

Omary alisema kuwa baadhi ya majengo ya madrasa na mabweni ya wanafunzi siyo rafiki kwenye miundombinu yake hali ambayo imekuwa ikitishia usalama wa mazingira yake.

"Nimesikitishwa na hali ya majengo ambayo siyo rafiki kwa upande wa mazingira yake,hivyo ninaagiza walimu na wanafunzi hakikisheni mazingira yanakuwa mazuri hii pia inatusaidia kuepukana na magonjwa ya mlipuko," alisema.

Mwenyekiti huyo aliyataja baadhi ya majengo hayo ya madrasa yaliyopo ambayo yanahitajika kuchukuliwa hatua thabiti ya kuhakikisha mazingira yake yapo kwenye hali ya usafi.

Hata hivyo, alisema kuwa ukaguzi ambao uliofanyika kwenye majengo hayo ni endelevu kwa ajili ya kuweka mazingira kwa muda wote kuwa rafiki kwa watumiaji wa miundombinu yake.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa kamati ya afya Bakwata wilaya ya Dodoma, Shekhe Said Gwazai, aliwataka wanafunzi wa madrasa kusoma kwa bidii ili waweze kuifahamu elimu ya dini ya kiislamu.

Alisema kuwa wakisoma kwa bidii wataweza kuwa viongozi wenye hofu ya Mungu na Taifa kwa ajili ya kutetea maslahi ya watanzania bila kujali itikadi yoyote ya kidini,kisiasa,rangi wala kabila.

**"Nimesikitishwa na hali ya majengo ambayo siyo rafiki kwa upande wa mazingira yake,hivyo ninaagiza walimu na wanafunzi hakikisheni mazingira yanakuwa mazuri hii pia inatusaidia kuepukana na magonjwa ya mlipuko," alisema**





# Mazrui: Bima ya afya muhimu sana kwa sasa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, amesema kuwa Mfuko wa Bima ya Afya ni muhimu sana hasa kwa wakati huu ambao huduma za afya zinatanuka zaidi na gharama zinakuwa kubwa zaidi.

Kutokana na hali hiyo, Waziri Nazrui alisema bima itasaidia wananchi kupata huduma za afya.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kufungua mkutano wa taasisi ya Phamaaccess uliofanyika mjini Zanzibar ambapo taasisi hiyo imetimiza miaka 20 tokea kuazishwa.

Alisema ingawa baadhi ya wananchi wa Zanzibar wana bima ya afya, lakini Serikali haijaanzisha bima ya afya, hivyo wakati umefika sasa wa serikali kuwa na bima ili wananchi kunufaika.

Alisema Phamaaccess ni washirika wazuri katika masuala ya afya na wazoefu wameshafanya kazi nchi mbalimbali za Afrika na wanauzoefu wa kutosha, hivyo kuja Zanzibar ni fursa kubwa kwa serikali. Alisema mafunzo wanayotoa yatasaidia kutumia njia sahihi za kutumia kuanzisha mfuko wa huduma ya bima ya afya Zanzibar ili kila Mzanzibari afaidike na afya bora.

"Afya bora ya Wazanzibari itapatikana pale patakapokuwa na huduma bora kwa mteja na itapatikana kila mzanzibari atapokuwa na kadi ya bima ya afya, ambayo itamuwezesha kupata huduma safi za afya,"alisema.

Alisema kuwa Serikali ya Zanzibar itahakikisha inafungua bima ya afya kwa madhumuni ya kuwasaidia wananchi kupata afya bora kwa kila Mzanzibari.

Akizungumzia kuhusu wimbi la nne ya ugonjwa wa Uviko 19, Waziri Mazrui alisema hadi sasa Zanzibar hakuna hata mgonjwa mmoja wa corona na Serikali inaendelea na jitihada za kupambana na wimbi la nne la ugonjwa huo.

Alisema hivi sasa kila mgonjwa anaefikishwa hospitali ambae anadalili ya mafua hupimwa corona na kuwataka wananchi kuendelea kufuata masharti ya watalamu wa afya katika kujikinga na ugonjwa huo.

Alisema kuwa wananchi watakapojikinga na corona uchumi utaimarika kwa sababu watalii na wawekezaji wataingia nchini baada ya kuona nchi ipo salama.

"Wimbi la nne la corona tusiliogope tulikabili kwa kujikinga na inshallah tutavuka salama kama tulivyovuka katika wimbi la kwanza, lapili na la tatu,"alisema Mazrui.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Phamaaccess Heri Marwa, alisema lengo kuu la taasisi hiyo ni kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wananchi ambapo watu wengi wanashindwa kuzifikia huduma za afya na wale wanaozifikia wengine huingia katika umasikini kwa sababu ya kulipia huduma za afya.

"Kwenye uwezeshaji wa huduma za afya Serikalini tumeshapeleka timu ya watalamu wa afya nchini Rwanda kwenda kujifunza na tunatarajia Rais wa Tanzania mwakani atazindua bima ya afya ya Serikali,"alisema Mkurugenzi huyo.



Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Lela Muhammed Mussa (kushoto), akiangalia bidhaa mbalimbali katika maonyesho ya wajasiriamali, katika maadhimisho ya Siku ya Mji Mkongwe yaliofanyika Forodhani, Mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Maadhimisho siku ya Kiswahili kila mwaka

**Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TUME ya Taifa ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO ) ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imesema Tanzania itaanza kuadhimisha mwaka huu siku ya Kiswahili Duniani Julai 7 kila mwaka.

Imesema uamuzi huo umefanyika baada ya Kiswahili kuingizwa katika Lugha za Kimataifa na Umoja wa Mataifa.

Hayo yalielezwa na Katibu Mtendaji wa Tume hiyo, Profesa Khamisi Mrembo, alipokuwa akizungumza katika maadhimisho ya kwanza ya siku ya Mji Mkongwe yaliyoanzishwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussen Ali Mwinyi, yaliyofanyika Ngome Kongwe Mjini Zanzibar

"Nataarifa njema napenda kuwaeleza tumepambana na kufanikiwa kuingiza lugha ya Kiswahili kuwa lugha inayotambuliwa na Umoja wa Mataifa na sasa tutakuwa tukisherekea Siku ya Kiswahili Duniani kila tarehe 7 mwezi wa 7 kila mwaka." alisema Prof. Khamis.

Alisema kutumika kwa lugha ya Kiswahili duniani kutasadia Tanzania kujitangaza kimataifa pamoja na kuongeza ajira kwa Watanzania kufundisha lugha ya Kiswahili katika mataifa ya Ulaya na Afrika.

Prof. Khamis alisema Tanzania mpaka sasa ina maeneo saba ya hifadhi ambayo yamekuwa kivutio kikubwa kwa watalii wanaotembelea Zanzibar ikiwamo hifadhi ya Mji Mkongwe wa Zanzibar.

Aliyataja maeneo hayo ni hifadhi ya Taifa ya Seregenti, Ngorongoro, Kilimanjaro, michoro ya miambani ya Kondoa na magofu ya Kilwa na songo mnara na pori la akiba la Selous.

Alisema kuwa Tume ya Taifa ya UNESCO ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeanzishwa kwa ibara ya 7 ya Katiba ya Shirika hilo ikitekeleza majukumu yake Zanzibar na Tanzania bara.

Alisema majukumu ya tume ni kuhakikisha maeneo ya hifadhi yanasimamiwa sawasawa ikiwemo hifadhi ya mji Mkongwe wa Zanzibar pamoja na hifadhi za wanyamapori, misitu na mambo ya kale katika hifadhi za Tanzania bara.

Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Idrisa Kitwana Mustafa, alisema

Rais Mwinyi aliamua kuanzisha siku hiyo baada ya kukutana na wadau wa Mji Mkongwe kujadili mkakati wa uendelezaji na uhifadhi wa Mji Mkongwe Desemba mwaka 2020.

# Wanahabari wakumbushwa kukemea udhalilishaji kijinsia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Internews Tanzania limesema kuwa waandishi wa habari wana nafasi kubwa ya kukemea ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa kutumia taaluma yao.

Kadhalika, shirika hilo limesema kwamba vitendo vya udhalilishaji kijinsia vimekuwa vikiathiri kiakili, kimwili na kisaikolojia.

Akifungua mafunzo kwa waandishi wa habari kuhusu siku 16 za kupinga ukatili na udhalilishaji wa kijinsi mafunzo ambayo yamefanyika kwa njia ya mtandao (ZOOM), mwezeshaji wa masuala ya habari kutoka shirika hilo Alakok Mayombo, alisema kuwa vitendo hivyo vimekuwa ni tishio kubwa kwa jamii, hivyo ni vyema waandishi wa habari kuvikemea.

Alisema iwapo waandishi wa habari kupitia vyombo vya habari watatekeleza wajibu wao wa kuisemea jamii matatizo hayo ambayo yamekuwa yakiwaathiri wanawake na watoto, itasaidia kupungua au kuondokana kabisa na kuwa na jamii inayoishi bila ya udhalilishaji.

Alisema waandishi wa habari wana fursa ya pekee ya kuleta mabadiliko kwa haraka katika jamii na iwapo wataitumia vyema fursa hiyo uwezekano wa kukomesha vitendo vya ukatili na udhalilishaji katika jamii ni mkubwa.

"Vyombo vya habari tunaamini kwamba kwa kalamu zetu tunaweza kufanya jambo na likaleta matunda kwa sababu tunayo fursa ya kuifikishia jamii taarifa kwa wakati," alisema Alakok.

Alieleza kuwa ufikishaji wa taarifa sahihi kwa jamii juu ya madhara ya vitendo vya ukatili wa kijinsia utasaidia kwa kiasi kikubwa kufikia lengo la kukomesha vitendo hivyo.

Aidha, aliwataka waandishi wa habari kuzitumia siku hizi 16 za kupinga ukatili kwa kujitafakari ili kubaini kwa namna gani wanachangia kupambana na vitendo vya udhalilishaji.


"Hii ni fursa nzuri kwa vyombo vya habari kutafakari mchango wetu katika kusaidia kwenye mapambano dhidi ya ukatili na kuleta mabadiliko kwenye jamii zetu," alisema.

Naye mwezeshaji wa mafunzo kutoka taasisi hiyo , Ali Sultan, aliwataka waandishi kutumia taaluma na ujuzi walionao kubuni mawazo na kuandika habari zinazolenga kuleta mabadiliko kwenye jamii.

Akizungumza katika mkutano huo ambao uliwashirikisha wadau wengine wa habari, Hatib Kibwana Mwenyekiti wa serikali ya mtaa Tandale, aliipongeza taasisi ya TIBA, Internews na waandishi wa habari kwa kusaidia kupambana na ukatili kwa watoto wa kike katika kata yake.

Alisema: "Tunaishukuru sana TIBA kupitia mradi wake wa 'Kijiwe cha Kahawa' imesaidia tumepaza sauti kuhusu watoto wetu wa kike kufanyiwa udhalilishaji kutokana na kata yetu kukosa shule ya sekondari na sasa serikali imekubali kujenga shule hapa." alisema.

Mafunzo hayo kwa wandishi wa habari kuhusu habari za udhalilishaji yaliyoandaliwa na shirika la Internews ni mwendelezo wa shirika hilo kuungana na wadau wengne ulimwenguni katika kampeni ya siku 16 za kupinga ukatili kwa wanawake na wasichana ambayo kwa mwaka huu inatimiza miaka 30 tangu kuanzishwa.



TUNDA
UKURASA 12



Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT





## UTATA MISS TANZANIA

# maswali mengi kuliko majibu, kushindwa kwenda Miss World

WAKATI mwakilishi wa Tanzania katika shindano la urembo la dunia, Juliana Rugumisa, akishindwa kwenda kushiriki shindano hilo nchini Puerto Rico, utata huo umeibua maswali mengi ambayo hayana majibu.

Juliana alitakiwa kujiunga na warembo kutoka mataifa mbalimbali ili kupigania taji la urembo ambalo shindano lake litafanyika Desemba 16, mwaka huu.

Katika taarifa iliyotolewa na waandaaji wa Miss Tanzania, imesema kwamba kutosafari kwa mwakilishi wa Tanzania ni kukosa visa ya kuingia nchini humo kutokana na changamoto ya ugonjwa wa Virusi Korona (UVIKO19).

"Tarehe 3 Desemba, 2021 ndio mwisho wa kuingia kambi ya Miss World baada ya nchi nyingi kupata changamoto ya kuchelewa kupata visa ya Marekani kwa wakati. Miss World wakaongeza muda na kuruhusu hadi ikifika hiyo kesho iwe mwisho." imeeleza taarifa hiyo.

Ikaongeza taarifa hiyo, "Hii ndio kusema kwa mwaka huu haitawezekana tena, hata hivyo mwisho wa mashindano ndio mwanzo wa mashindano yajayo, tunashukuru sana wadau wetu Miss World kwa jitihada kubwa na kuhakikisha hadi tunapata ahadi ya mapema badala ya Januari."

Hata hivyo, taarifa hiyo imeonyesha udhaifu mkubwa wa kimaelezo baada ya suala hilo zito ambalo linagusa nchi, kuelezwa juu juu kiasi ambacho watu wamebaki na maswali mengi ambayo hawakuweza kupata majibu.

Kwanza kamati ilitakiwa kueleza kwa nini visa ya mwakilishi wetu haikupatikana ikiwa nchi nyingine wamepata na warembo wao wamefanikiwa kujiunga katika kambi na hatimaye kushiriki shindano.

Pili, suala la Uviko-19 linatambulika duniani kote na kila nchi imeweka utaratibu wa kuingia katika kuidhibiti, na sharti kubwa ni kulazimisha kila mtu anayengia ndani ya nchi husika, lazima apate chanjo na aonyeshe cheti cha kuthibitisha. Kamati ya Miss Tanzania ingetueleza kama mwakilishi wetu hakupata chanjo au kama kuna tatizo lingine la kiafya.

Tatu, katika taarifa yao wamechanganya watu wakisema visa ya Marekani imekuwa ngumu kuipata, lakini ikumbukwe shindano la Miss World linajulikana na kongwe, hivyo inakuwa vigumu kwa mshiriki aliyekidhi vigezo vyote Marekani inamkataa.

Hayo ni baadhi tu ya maswali ambayo kamati ya Miss Tanzania imeshindwa kuyapa majibu ili kuondoa wasiwasi Watanzania ambao walipenda kuona mwakilishi wao akipanda jukwaani na kutoa ushindani. Kuna umuhimu kwa wahusika kusema ukweli ili kama kuna sehemu kulifanyika uzembe ichukuliwe hatua inayostahili.

BASI SAWA

## Mariam Mungu atakubariki

MWIMBAJI nyota wa Injili nchini Mariam Kilyenyi, anatarajia kuiweka wakfu kampuni yake ya Glorious MK Promotion katika kanisa la Power Of Word linaloongozwa na Mchungaji Bahati Bukuku, eneo la Tabata jijini Dar Es Salaam..

Akizungumza na BT, Mariam amesema shughuli ya kuweka wakfu itaambatana na ibada ya shukrani ya kutimiza miaka mitatu ya huduma yake ya uimbaji.



"Chini ya kampuni hii nimeweza kufanya kazi na waimbaji wengi wakubwa kwa wadogo kuhakikisha muziki wao unawafikia watu wengi Zaidi, pia nimeweza kutangaza makanisa, mikutano na matamasha mengi yaliyofanikiwa kwa kiasi kikubwa na sasa ni muda wa kuisimika rasmi ili Mungu aendelee kuitumia kama chombo chake," amesema mrembo huyo

## Biraza awakumbusha Fungua Moyo Wako



MWANAMUZIKI wa kizazi kipya anayekuja kwa kasi, Venance Biraza, amewaomba wapenzi wa muziki mzuri kuipokea video ya wimbo wake mpya, Fungua Moyo Wako.

Biraza ameliambia BT kuwa baada ya kimya cha muda mrefu amerudi kivingine na wimbo huo ambao tayari upo kwenye chati mbalimbali za muziki nchini.

"Nashukuru Mungu kwa kuniwezesha kuachia wimbo huu ambao unafanya vizuri kwa sasa, naamini watu wengi watabarikiwa ila niwaombe mashabiki waingie kwenye chaneli yangu ya YouTube kuna video watafurahia," amesema Biraza.



## Tunda maneno yanaumba

MPAMBAJI wa video za muziki, Tunda amebadili msimamo wake wa kujiondoa uhai endapo mwaka huu unaofika ukingoni hataolewa, na badala yake amesema kuna vitu vimemshawishi kubaki duniani.

Tunda ambaye ni mchumba wa mwanamuziki wa Bongo Fleva, Whozu Cappuccino, kutokana na mambo mengi yamemfanya kushawishika, ahadi hiyo anaipeleka mbele hadi mwakani.

Nilisema mwaka huu nisipoolewa najiua, kuna marekebisho ya kiufundi yamejitokeza nasogeza hadi mwakani mwezi kama huu". Amesema kupitia ukurasa wake wa Instagram.

## Matilda: Binadamu hupanga, Mungu hupangua

**Na Adam Fungamwango**

HAPA duniani chochote kinawezekana. Unaweza ukaona kama kuna kitu fulani si rahisi kufanyika kutokana na mazingira yaliyopo, lakini ukweli ni kwamba hakuna ambacho kinashindwa kufanyika.

Na ukitaka kuamini hilo, hebu ifuatilie hii filamu ya 'Matilda' Imechezwa na baadhi ya wasanii mbalimbali maarufu kama Mzee Jengua, Salma Jabu 'Nisha', Wellu Sengo, Hemed Suleiman, Kikumba na wengine wengi.

Nisha ni mfanyakazi wa kampuni moja binafsi, anapata matatizo ya kushindwa kulipa kodi, kitu kinachosababisha kumuomba Hemed ambaye anaelewana naye, amsaidie kwa bosi.

Hemed anafanya hivyo na bosi anampa hiyo pesa kwa ajili ya kodi. Lakini wakati Nisha anaondoka anapewa lifti na bosi, ambaye anataka kutumia msaada huo kuomba penzi.

Badala ya Nisha kupelekwa kwake, anapelekwa nyumbani kwa bosi wake na kuomba penzi kinguvu. Nisha anakimbia, kesho yake tu akapewa barua ya kuachishwa kazi.

Anaporudi nyumbani anakuta tayari ameshatolewa vitu nje.

Alichofanya ni kumpigia Hemed ambaye alimtaka aende kwake. Huko alipata hifadhi. Pamoja na kuishi hapo, Hemed hakushawishika na Nisha, badala yake akaangukia kwenye penzi na msichana mwingine mcheza shoo aitwaye Matilda.

Wazazi wa Hemed wao walivutiwa mno na Nisha na kumlazimisha kijana wao amuoe, lakini ilishindikana.

Kilichotokea ni kwamba Hemed alimpa mimba Nisha na kumkimbia kwenda kupanga nyumba nyingine, akaishi na Matilda.

Nisha anafukuzwa kwenye nyumba kwa kukosa kodi, anaingia mtaani na kuanza kubangaiza, akifanya biashara ya kuuza vitumbua, akilea mimba yake, hadi alipojifungua.

Maisha ya Hemed na Matilda yalikuwa kama ya maigizo. Siku moja akamtukana bosi mmoja wa kike wa kampuni yao, akidhani ni mmoja wa maharawa zake. Hiyo ilitosha Hemed kufukuzwa kazi. Ukazuka




ugomvi mkubwa baina yao na kusababisha Matilda akasirike na kumchukua mtoto usiku kuondoka naye.

Njiani anakutana na watu wabaya, wanambaka. Mtoto anapotea, lakini akaanguka kwenye mikono ya Nisha ambaye naye ana mtoto wa Hemed.

Matilda anasaka mtoto na kufanikiwa kumpata akiwa kwenye mikono ya Nisha. Katika kuulizana wanajikuta wanafahamiana kuwa ni mtu na dada yake wa baba na mama mmoja.

Wote wamezaa na Hemed kila mmoja mtoto mmoja wa kiume.

Matilda baada ya kubakwa anapimwa na kukuta ana maambukizo ya Ukimwi, hivyo anamchukua mdogo wake Nisha na kumpeleka kwa Hemed, akimwambia kuwa amuoe badala yake, ili alee watoto. Matilda anajiua kwa kunywa sumu.





## Ukimkataa Roma, utabaki na ndoto tu

RAPA Roma Mkatoliki, ametoa maoni yake kuwa kamwe mabifu ya wasanii wa bongo, hayawezi kufananishwa na wanamuziki TuPac na Big Notorius.

Amesema pamoja na wasanii wengi kuwa na ugomvi, chuki, husda, bifu na kulipizana visasi, lakini kamwe haitafikia hatua kama ya wakali hao wa Marekani ambao vifo vyao vilitokana na ugomvi wao.

"Ni kweli kuna wasanii wa home wana ugomvi,chuki,husda,visasi,bifu lakini haitaweza kufika hatua ya kina TuPac, Bongo kuna kaupendo bado kapo" ameandika.

## DUNIA YA WALIMWENGU

**Na Adam Fungamwango**

UKISIKILIZA hadithi nyingi na mambo mengi ya zamani na hata ukisoma kwenye vitabu mbalimbali vyenye kuheshimika, utagundua hakuna kitu kipya hapa duniani kinachofanyika.

Yote ni yale yale tu. Ni kama vile wanasayansi wanavyosema dunia inajizungusha yenyewe kwenye mhimili wake na kweli yote yanayofanyika yanajirudia tu.

Tena kuna vitu vingine vilifanyika zamani hadi leo hii havijafanyika tena. Vinavyoendelea kujirudia ni baadhi ya mambo machache tu yaliyofanyika miaka milioni nyingi huko nyuma.

Ndiyo maana utasikia watu wanakwambia maisha ya sasa ni magumu. Lakini ukisikia nyimbo za miaka 50 nyuma, utakuta wanaimba maisha ya sasa ni magumu. Ina maana yalianza kuwa magumu tangu zamani. Hivi sasa kuna udanganyifu wa mapenzi. Ukisoma vitabu vya miaka mingi nyuma, utakuta pia kulikuwa na udanganyifu.

Leo mada hii tutaziangalia nyimbo ambazo zinazungumzia dunia, raha, matatizo yake na vituko zilizotungwa miaka ya 1980 mwanzoni hadi mwishoni.

**Dunia Duara-Shaaban Dede**

Shaaban Dede akiwa na Bima Lee, alitunga kibao cha 'Dunia Duara'. Hiki kinazungumzia juu ya mtu anayechekwa na wenzake kuwa hana kitu.

Lakini mwenyewe anajipa matumaini kuwa dunia ni duara na huzunguka, hivyo anajua kesho atapata kwa jinsi anavyojituma. Anasema jua halina mpaka, huangaza pote kwa hiyo ipo siku na yeye ataangaziwa, kwani kama samaki baharini, wadudu mapangoni na wanyama porini wanaishi, basi kwa kudra za Mungu na yeye atapata tu.

**Dunia Uwanja wa Fujo-Marijani**

Jabali la Muziki Marijani Rajab, yeye akatunga kibao cha 'Dunia Uwanja wa Fujo'. Anawatahadharisha wote wanaojimwambafai na kuiona dunia kama yao, kuwa walikuwepo watemi, wafalme wenye nguvu, lakini leo hii hawapo.

Alikuwepo Firauni, Hitler, Nduli Idd Amini ambao historia inasema ni moja kati ya viongozi wababe kuwahi kutokea duniani, lakini kwenye dunia hii hakuna mbabe kushinda Mwenyezi Mungu.

Kwa maana hiyo anawaasa watu hususan wanaopewa dhamana, kuishi vizuri na watu, kwa sababu ubabe hauna maana, akamalizia kwa kusema kwenye dunia hii 'kula ugali wako ukalale'.

**Dunia-Remmy Ongalla**

Remmy Ongalla kwenye fasihi yake ya wimbo huu wa 'Dunia' anasema yote ambayo binadamu atayafanya hapa duniani, ikiwa ubaya au wema, atalipwa hapa hapa ulimwenguni.

Anasema kwa Mungu hatupajui, hivyo binadamu anatakiwa kutenda wema, kwani kuna baadhi ya watu hudhulumu wengine kwa vyeo vyao, wadhifa, pesa na umaarufu.



**Dunia-TX Moshi William**

Akiwa na bendi ya Polisi Jazz, kabla ya kujiunga bendi ya Juwata Jazz, alitunga kibao kisemacho 'Dunia'. Anauliza, mwezi na nyota usiku zinang'aa bili yake analipa nani? Na ilitakiwa kabisa aulizwe anayelipwa bili ni nani? Huyo ni mwenyezi Mungu. Yeye kila kitu hutoa bure kwa waja wake.

**Dunia Imani Imekwisha-Marijani**

Hapa Marijani amerudi tena hapa na wimbo wa 'Dunia Imekwisha'. Yoyote aliyedhani eti sasa ndiyo kuna dhana hiyo, lakini hata miaka ya 1970 hadi 1980, kulikuwa na matendo kiasi cha kuonekana dunia imani yake ni ndogo. Watu wanaibiana, Wanatapeliana, Wanadhulimiana. Kuna wanaodhulumu watoto yatima. Wanaotaka kuwaua wazazi wao ili warithi mali na mengine mengi.



# R Kelly huu ni mwaka wake

MWAKA 2021, umekuwa mchungu kwa mwanamuziki wa Marekani R. Kelly, ambaye licha ya kusubiri hukumu yake baada ya kupatikana na hatia ya unyanyasaji wa kingono, sasa anakabiliwa na tuhuma ya kujaribu kuficha ukweli.

Katika ripoti mpya inaonyesha R Kelly na meneja wake wamejaribu kuwatisha na kuwanyamazisha wanaodaiwa kudhulumiwa kingono.

Kulingana na mtandao wa PageSix, wote wawili wanadaiwa kujaribu kuwatisha kwa mbinu ambazo ni pamoja na kupiga simu za vitisho.

Wanawake watatu waliohusika, Lizette Martinez, Lisa Van Allen na Faith Rogers ambao wanadai walidhulumiwa kingono na mfungwa huyo mwenye umri wa miaka 54, walifungua kesi katika Mahakama ya Juu ya Manhattan wakidai kuwa R Kelly alipigwa picha akihudhuria kikao tofauti cha mahakama huko Chicago mapema Septemba

"Kelly na watu wake wa ndani walianza juhudi zilizoratibiwa kunyamazisha, kunyanyasa, kuhonga na kuwatisha wale vijana wa kike na marafiki na familia zao." ilidai ripoti hiyo.



## Kanye unazidi kuwachanganya

RAPA Kanye West na mkewe waliyetengana Kim Kardashian, walijikuta wakikutana uso kwa uso baada ya wote wawili kuhudhuria katika hafla ya kuaga mwili wa mwanamitindo marehemu Virgil Abloh.

Hata hivyo, wenzi hao walionekana kuwa pamoja katika hafla hiyo wakiwa na binti yao wa kwanza, North West.

Kumbukumbu hizo zimefanyika katika msimu wa mchipuko huko Miami nchini Marekani.

Kardashian na West walikaa mstari wa mbele kwenye mkusanyiko huo wa kumkumbuka Abloh ambaye alikuwa mahiri katika ubunifu wa mitindo duniani.

## Common miaka miwili inatosha

MWANAMUZIKI wa Marekani Common na mpenzi wake Tiffany Haddish, hatimaye wameachana baaada ya uhusiano wao kudumu kwa miaka miwili.

Vyanzo vya uhakika vinasema wawili hao wameachana siku chache zilizopita na kila mtu ana mambo yake.

"Hawapo katika mji mmoja kwa sasa, kila mtu yupo na mambo yake ," kilisema chanzo hicho.






## Rihanna umemaliza mwaka vizuri

MSANII wa muziki kutoka Barbados, Rihanna, ameweka rekodi kuwa mwanamke wa pili kupewa tuzo ya juu ya kitaifa inayomtambua kama mtu aliyekipa sifa kisiwa hicho.

Tuzo hiyo ya heshima ya Rais wa Barbados, Dame Sandra Mason, ambaye alimwagia sifa kwa kumtaja kama madini ya almasi inayoangazia nchi hiyo.

"Kwa niaba ya taifa, tunatoa shukrani kwako, watu wanajivunia zaidi, tunamkabidhi shujaa wa taifa la Barbados, Balozi Robyn Rihanna Fenty. Uendelee kung'aa kama almasi unapoleta heshima kwa taifa lako kwa maneno yako, kwa matendo yako, Mungu akubariki, mpenzi wangu," amesema.

## Lindsay tembo hazeeki maini

MWIGIZAJI mkongwe wa Marekani, Lindsay Lohan, hatimaye amefunga ndoa na mpenzi wake Bader Shammas.

Mtoto wa msanii huyo nyota wa filamu, alitoa taarifa katika ukurasa wake wa Instagram, kwamba mama yake alifunga ndoa Novemba 28.

"Mpenzi wangu, maisha yangu, familia yangu na jicho langu kwa maisha yajayo Bader Shammas," ameandika Lindsay.



## NYUMBA NI CHOO

# Watafiti wasema nusu yake nchini hazijafikia kiwango kinachohitajika

## ●Njombe yaongoza kwa hatua bora

**Na Christina Mwakangale**

UTU wa binadamu una tafsiri iliyoko katika nyanja tofauti, zikiwamo za afya ambako kunahitajika huduma muhimu ndani ya jamii hadi familia kama maji na vyoo.

Vyoo bora na vya kisasa, daima vinatajwa kusaidia kutoenea magonjwa ya kuambukiza kama vile kuhara, kipindupindu na kutunza mazingira.

Ripoti ya utafiti iliyofanywa kuhusu Bajeti ya Kaya Mwaka 2017/18, takwimu nchini zinataja asilimia 47 ya Watanzania wanatumia vyoo vilivyoboreshwa, wakiwamo wanaoishi jijini Dar es Salaam.

Ni hali inayoonyesha kaya zenye vyoo bora nchini, zinaongozwa na mkoa wa Njombe ambao ndiyo uko juu zaidi ukiwa na asilimia 46.3 ya vyoo bora kitaifa; Kilimanjaro ina asilimia 43.3; Morogoro (asilimia 35.1) Dar es Salaam (asilimia 33.5) na Mbeya (asilimia 32.1)

Ofisa Afya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Reginald Mlay, anasema mikakati ya takribani miaka 10, imelifanya jiji kuongoza jitihada za kuwa na vyoo bora na kuondokana na utiririshaji maji machafu.

Anasema kampeni ilizinduliwa mwaka 2012 jijini Dar es Salaam, ili kuinua kiwango cha usafi wa mazingira na kuepuka utiririshaji maji machafu, ambao ulisababisha mlipuko wa magonjwa, ikiwamo kipindupindu.

"Usafi wa mazingira ulianza mwaka 2012, katika kata za jiji 13 na mitaa 26, baadaye zilijiunga nyingine ikawa na kata 36 na mitaa 159. Kampeni hii ilitokana na mkakati wa kupiga hali ya magonjwa ambayo pia ilijitokeza miaka ya 1972 ikaanzishwa 'Mtu ni Afya'," anasema.


Mlay anasema, majukumu yanayotekelezwa sasa. Miaka hiyo ilikuwa ni kutoa elimu, ujenzi wa vyoo kila kaya na sehemu maalumu ya kunawa mikono.

"Mfumo wa maji taka unasaidia kutotiririshwa maji machafu na kusababisha maradhi. Kuna maeneo ambayo yalijengwa mfumo wa kupokea maji taka, yaani mabwawa kama vile Kipawa, Vingunguti, Buguruni huku kulikuwa na magonjwa ya mlipuko sana, sasa imekuwa ni historia," anasema Mlay.

### MAFANIKIO YALIKOFIKA

Kuhusu mafanikio tangu kampeni ya jiji Dar es Salaam, Mlay anafafanua kwamba tangu mwaka 2012 hadi Septemba mwaka huu, asilimia 95 ya ujenzi wa vyoo bora imefikiwa.

Anasema elimu ya kunawa mikono imeongezeka kutoka asilimia nane hadi 67 ya kaya zote zina sehemu ya kunawa mikono, huku halmashauri ya jiji, ikiendelea kutoa vyoo kwenye kaya maskini, hadi sasa jumla ni 729.




Shughuli za kuhudumia choo zikiendelea katika sura tofauti. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Kadhalika, mpango huo wa kutoa vyoo ambao jiji unashirikiana na wadau mbalimbali, pia umezifikia shule 42 na kupatiwa vyoo 615 pamoja na eneo la jengo maalumu kwa ajili ya kubadilishia taulo za kike wasichana.

Mlay anasema, zipo changamoto kwenye mpango huo ambao ni uhaba wa maji katika vyoo vilivyopo shuleni na penye kaya, pia kikwazo ni usafiri kwa maofisa afya kuyazungukia maeneo yaliyopo kwenye mpango huo, kubaini maendeleo.

### KULIVYO WILAYANI

Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu Ludigija anasema ni muhimu hadhi ya jiji la Dar es Salaam, iendane na makazi pamoja na maeneo ya biashara yenye vyoo bora.

Ludigija akipokea vifaa vya kufanya usafi kutoka shirika la WaterAid, kwa ajili ya Kituo cha afya Mama naMtoto Chanika (Nguvu Kazi) pamoja na Buguruni, kuadhimisha Siku ya Choo Duniani, akisema jiji kwa kushirikiana na wadau kupitia kampeni ya usafi wa mazingira imefanikisha kufikia asilimia 95.4 ya malengo asilimia 70.

"Zamani tulishihudia maradhi ya mlipuko kama kipindupindu kutokana na utiririshaji maji machafu. Ndio maana yalijengwa mabwawa maji ya kutunza maji machafu kwenye baadhi ya maeneo kulikokithiri magonjwa.

"Kwa miaka mitano hatujashuhudia magonjwa ya mlipuko. Tutahakikisha kila kaya Ina vyoo bora. Ujenzi wa kila nyumba uzingatie uwepo wa choo kuendana hadhi ya jiji," anasema Ludigija.

### KINACHOJIRI DUNIANI

Ripoti ya Mpango wa Benki ya Dunia na Usafi ya Mwaka 2012, inasema kutokuwapo usafi kunasababisha Tanzania kuingia gharama ya shilingi bilioni 301 kila mwaka.

Lengo Namba Sita la Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa - SDG, ni ifikapo mwaka 2030 upatikanaji wa maji safina salama, lifanikiwe, huku watoto 800 wakikadiriwa kupoteza maisha kutokana na kuhara, usafi duni na unywaji wa maji yasiyo safi na salama na kwamba kukosekana maji huathiri zaidi wasichana na wanawake.

### WADAU KAMPENI

Mkurugenzi Mkazi wa shirika la Wateraid, Anna Mzinga, katika kuadhimisha Siku ya Choo Duniani, inayoadhimishwa kila Novemba 19 ya mwaka duniani kote, limetoa vifaa vya usafi kwenye Hospitali ya Mama na Mtoto Chanika na Kituo cha Afya Buguruni.

Anasema, pia limetoa vifaa vya usafi kwa kikundi kiitwacho Hekima Kwetu, kupitia kampeni yao ya 'choo safi, hadhi yangu', vilivyotolewa ni pamoja na fagio, sabuni, mikokoteni, buti, jaketi ang'avu, glovu ngumu, fagio na vifaa vingine vyenye thamani ya Sh. Milioni 10.

"Kama sehemu ya maadhimisho ya siku hii yenye kaulimbiu ya "kipe hadhi chuo chako", kundi hiki cha 'Hekima Kwetu' kinashirikiana na na ofisi ya halmashauri ya jiji, kwa pamoja wanafanya usafi katika maeneo ikiwamo shule za msingi nane, zilizopo katika wilaya ya Ilala.

"Ripoti ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2020 mafanikio yanaonyesha asilimia 66 ya kaya Tanzania wana vyoo bora majumbani ukilinganisha na asilimia31 mwaka 2016," anasema

Mkurugenzi huyo anasema shirika hutoa mafunzo namna ya kujenga vyoo bora na stahimilivu. pamoja na kujenga kwenye baadhi ya maeneo nchini na usalama, ikitoa vifaa vya usalama na usafi kwa wafanya usafi wa vyoo, ikiwa sehemu ya kampeni za kitaifa, ikiwamo ya vyoo bora.

Anna anasema, kuna hitaji la kuendelea kuhamasisha ili ifikapo 2030, kila nyumba iwe na choo bora. Pia, kauli mbiu ya mwaka huu inaangazia jukumu la kutoa kipaumbele na kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya vyoo ikiwemo mifumo bora ya maji na vifaa vya usafi wa vyoo.

"Suala la vyoo linamgusa kila mmoja wetu bila kujali hadhi na hali. Watoa uamuzi katika ngazi mbalimbali za serikali, watekelezaji na wadau, tunaomba sote tufanikishe haya matatu; kwanza - vyoo bora, pili uwapo maji chooni na tatu vifaa vya kunawia mikono baada ya kutoka chooni.

"Vyoo bora vya nyumbani, shuleni na vituo vya kutolea huduma za afya huwasaidia kutimiza uwezo wao na kutekeleza wajibu wao kikamilifu katika jamii, hasa wakati wa hedhi na ujauzito.

"Mfano, kukiwa na vyoo bora vyenye mifumo bora ya maji shuleni, wasichana hawatabaki nyumbani wanapokuwa kwenye hedhi kama ambavyo ripoti ya Hali ya Afya ya Hedhi na Usafi Miongoni mwa Wasichana," inafafanua



## TULIKOTOKA, TULIKO & TUNAKOELEKEA...

# Enzi waruka ukuta Uwanja Taifa, wasakata dansi nje ya ukumbi

**Na Adam Fungamwango**



Foleni ya wapenzi wa soka kuingia ndani wa Uwanja wa Benjamin Mkapa, ulio mpya jirani na mkongwe Uwanja wa Uhuru. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

UKIWA unatazama mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, wakati mwingine kamera huwa zinahamishwa uwanjani na kupelekwa kwenye matukio mbalimbali ndani na nje ya uwanja.

Moja ya mambo yanayowavutia watazamaji wengi, mbali na kuwa ni jambo la hatari sana ni pale wanapoonekana baadhi ya mashabiki wapo juu ya miti, lakini wanaangalia mpira.

Miti hiyo ni ile iliyopo nje ya uwanja, lakini baadhi ya mashabiki ambao hawajajaliwa kuwa na pesa za viingilio wakati huo, wanakuwa wamepanda juu ya miti na kung'ang'ania huko kila mtu na staili yake, ili mradi tu aweze kushuhudia mechi.

Mara nyingi huwa ni mechi zinazozihusu klabu kubwa mbili nchini zenye mashabiki wengi, Simba na Yanga. Ni timu zilizojaliwa kuwa na mashabiki wengi kila kona ya nchi, hivyo popote inapokwenda kucheza mikoani hujitokeza mashabiki wengi mno kutaka kuangalia mechi na kuona wachezaji, wakati mwingine kuliko hata Dar es Salaam.

Hiyo kwenye miti ni dibaji tu. Wapo wanaokuwa wamepanda kwenye maghorofa mbalimbali ambayo bado yapo katika hatua za ujenzi.

Nimeshawahi kuona baadhi ya mashabiki wameparamia nguzo kubwa za chuma za umeme, wako juu wakiangalia moja kati ya mechi za ligi kuu.

Nasema ni mambo ya hatari sana, lakini mashabiki wakati mwingine huwa kama 'vichaa' linapokuja jambo la mpira wa miguu, hasa timu wanazozipenda. Huwa hawajali.

Mikoa mingine utaona watu kwenye milima wakiwa wamekaa juu wakifuatilia mechi kama kawaida, kuna mikoa yenye mawe makubwa kama Mwanza na Singida. Nako utaona watu wapo juu ya mawe. Wametulia tuli, wanaangalia kabumbu.

Hiyo inanikumbusha miaka mingi nyuma. Miaka ya 1970 hadi 1980 na zaidi kabla na baada ya hapo, kwenye jiji la Dar es Salaam na mikoa mingine ambako watu wengi waliokuwa na kiu ya soka, lakini hawana uwezo wa kuingia walivyobuni mbinu kali ya kuruka ukuta na kuingia ndani licha ya ulinzi mkali wa askari polisi, waliokuwa na farasi na mbwa wakati huo.

Burudani ni pale wanapofika eneo la uwanja. Mashabiki wasio na viingilio hugawanyika vikundi. Wanapanda kila upande wa ukuta, hasa Kusini, Kaskazini na Mashariki kwenye Uwanja wa Uhuru wakati huo ukiitwa Uwanja wa Taifa, maeneo ambako kuna majukwaa ya kawaida.

Wote hao lengo ni moja tu kuruka chini na kuelekea uwanjani, wakajichanganye na wenzao walioingia kwa kiingilio wawe mashuhuda kamili wa mechi hizo.

Ni ujuzi wa aina yake, kwani ukuta wa Uwanja wa Taifa ni mrefu sana hata kwa mtu mzima kuparamia na kuruka chini upande wa pili ni ngumu sana na huko chini wanakotua kuna maafande waliokuwa wanalinda, pengine wana mbwa na nje kuna farasi na mbwa wengineo.

Wakishasheheni vya kutosha ukutani, ni kama wamekubaliana kwa mafunzo ya pamoja, maana ghafla mluzi utapigwa, upande mmoja wataruka chini kwa pamoja na kuanza kukimbia kuelekea kwenye majukwaa uwanjani.

Wakati polisi wanakuwa wamehamanika na kutaka kuwakimbiza na upande wa pili nao wanakuwa wamepata nafasi wanaruka pia. Ni hali iliyokuwa inawachanganya mno maafande, hivyo watu wengi wanaingia uwanjani bure.

Ni staili kama ya nyumbu. Wapo wachache kama wawili au watatu watakaokamatwa, lakini wengi wanafanikiwa kuvuka kuingia uwanjani. Walionasa walipata adhabu kidogo kama kuchapwa fimbo, kulazwa chali au kifudifudi wakati mechi inaendelea, lakini baadaye waliachiwa.

Inapokuwa mechi inayohusu Taifa Stars au nyingine za kimataifa kama za Klabu Bingwa Afrika au Shirikisho, basi husubiri upigwe wimbo wa Taifa ili waruke.

Upenyo mkuu waliotumia ni pale maafande wanakuwa 'wamekauka' kutii nyimbo mbili za Taifa ya nchini na wageni zikifuatana, hawawezi kuwakimbiza wakati wimbo huo unapigwa. Wanakuwa wamesimama tu kwa heshima zote.

Hapo maafande wakijipanga kukabili waruka ukuta hao ambao kwa kiasi kikubwa ni vijana wakiwafuatilia kwa macho, baadhi yao hadi wanakofikia na baada ya nyimbo kwisha, waliwafuatilia na kuwakamata, ndipo adhabu dhidi yao huanza.

Waruka ukuta walio na uzoefu au wajanja, walijisogeza kukaa mbali zaidi na waliko maafande na kila mara walibuni staili tofauti za kuwalaghai askari katika staili hizo za kuparamia ukuta ili kuingia uwanjani.

Watoto wadogo umri wa shule ya msingi katika zama za miaka ya 1970 walifaidika, maana waliruhusiwa kuingia bure. Lakini, baadaye, baada ya kukataliwa nao walijiunga na timu ya waruka ukuta. Kulikuwapo kundi lingine waoga wa kuruka ukuta, ambao walibaki nje kufuatilia mpira kutokana na sauti za kushangilia uwanjani, ikizingatiwa hata redio za mkononi wakati huo zilikuwa adimu.

Nao walikuwa na fursa zao inapotimu kati ya dakikia tano na 10 za mwisho waliruhusiwa, Hiyo ilijulikana sana kama 'fungulia mbwa.'

Tabia hiyo ya kuruka ukuta ilifika ukomo, pale alipoteuliwa mwanamama Fatma Said Ali kuwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Utamaduni, Vijana na Michezo. Sijui alikuwa anaona au anaambiwa vituko hivyo kwa watoto?

Yeye akaelekeza watoto wote kuanzia miaka 10 kurudi chini waingie bure mpirani, akilenga kuwafanya wapende zaidi soka wakiwa ilhali bado wadogo, waige yale wanayoyaona kwa wachezaji wakubwa uwanjani, ili taifa liwe na wachezaji wengi wazuri baadaye.

**KWENYE MUZIKI JE?**

Huko nako kulikuwa na 'jambo lake', kwani mambo hivyo hivyo. Wapenzi wengi wa burudani hiyo, hasa waliokosa uwezo wa kuwa na viingilio walikuwa wanakwenda hadi kwenye ukumbi muziki unakopigwa kumefurika ndani, wao wanakaa nje kusikiliza muziki wakiwa 'wameulamba' kimavazi na kulisakata kama walio ndani.

Dansi wakati huo ilikuwa burudani iliyoshika chati kitaifa. Waliofika kwenye ukumbi mathalani jijini Dar es Salaam wakati huo kama vile Wami Bar, Mwananyamala; Mundo Bar Temeke; Mkirikiti Msasani, Wapiwapi Chang'ombe, pia DDC Magomeni na Kariakoo ni mashuhuda hai.

Uzuri ni wakati huo kulikuwapo vyombo vya muziki aina ya 'Ranger' kutoka Italia, vilivyokuwa na nguvu kubwa ya sauti na kusikika kwa ufasaha hadi umbali kilomita 10 kutoka muziki unakopigwa, huku bendi nazo zikiwa na mafundi mitambo wataalamu waliotukuka 'kuiseti.'

Hicho nacho kilitawala kwenye maeneo ya burudani ya disko, zikiwa kwenye chati. Kulikuwapo waliosubiri wenzao watoke nje wakiwa wamepigwa muhuri mkononi ukiwa ndio utaratibu wa wakati huo.

Walio nje kwa kushirikiana na wa ndani penye burudani walibuni ujanja wa mkono uliopigwa mhuri unagandamiziwa kwa aliye nje baada ya kutoka kwa muda, hivyo naye anajifanya alikuwapo ndani na katoka nje mara moja.

Hapo alionyesha muhuri tena akijiamini kwa kiasi kikubwa anapita na kujiunga na wasakata dansi au disko ukumbini, ikiwa ni yaleyale ya waruka ukuta. Ama miaka 60 ya uhuru ina mengi ya kujivunia katika mabadiliko!



Ndio yalivyo maisha ya kuingia ukumbini kwa kupanda ukuta.

**Simu: + 255 716 350534**

## HABARI KIMATAIFA

## Kiongozi wa kijeshi aomba kuungwa mkono

**KHARTOOM,** SUDAN

KIONGOZI wa kijeshi wa Sudan Jenerali Abdel Fattah al-Burhan, ametoa wito kwa Umoja wa Mataifa kuunga mkono serikali ya mpito.

Jenerali Burhan juzi alikutana na mwakilishi maalum wa Umoja wa Mataifa nchini humo, Volker Perthes, ambaye alisema kupitia ukurasa wake wa Twitter kwamba licha ya kukaribisha mpango huo wa kurejeshwa kwa utaratibu wa kikatiba,hatua nyingine muhimu zinapaswa kufuata, hata hivyo hakufafanua zaidi.

Jenerali Burhan alisema atashirikiana na Waziri Mkuu wa kiraia aliyerejeshwa madarakani Abdalla Hamdok na kuunga mkono serikali ya mpito atakayounda hadi uchaguzi ufanyike.

Mapinduzi yaliyoongozwa na kiongozi huyo wa kijeshi Oktoba mwaka huu, yalipelekea kupinduliwa kwa serikali ya mpito na kuondolewa madarakani kwa Hamdok.

Waziri Mkuu huyo alirejeshwa madarakani mwezi uliopita baada ya kutia saini mkataba wa kumaliza mgogoro.

Hata hivyo, kila kukicha kunafanyika maandamano makubwa kuwapinga viongozi wa kijeshi ambao walifanya mapinduzi.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa António Guterres na Mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika, Moussa Faki, wamewataka wananchi kuunga mkono makubaliano hayo ili kurejesha demokrasia ya amani. Guterres alisema ingawa hali si kamilifu, ni hatua kuelekea demokrasia. **BBC**

## Baba ataka mshahara wa mtoto wake kufidia gharama za kumsomesha

**NAIROBI,** KENYA

MWANAUME mmoja nchini Kenya amemshtaki mwanawe ambaye pia ni mtu mzima akitaka apewe asilimia 20 ya mshahara wake kwa ajili ya kukidhi mahitaji yake ya kila mwezi.

Gideon Kisira Cherowo, 73, alidai amechukua hatua hiyo kama matunzo baada ya kuuza ardhi yake na mali yake nyingine kwa ajili ya kulipia masomo ya mwanawe hadi chuo kikuu.

Alidai mtoto wake huyo wa kiume ambaye sasa ana umri wa miaka 48, huwa hampi msaada wowote tangu apate ajira.

Familia ya Cherowo inaishi katika nyumba ya udongo katika kijiji chake magharibi mwa Kenya.

Gazeti la Daily Nation lilituma picha ya mwanamume huyo kwenye ukurasa wake wa Twitter, na kueleza kuwa mwanawe hajafika nyumbani kwa miaka 17 iliyopita na familia imeomba msaada wake bila mafanikio.

Cherowo aliambia mahakama kwamba hawezi kumudu huduma za wakili, lakini aliambatana na mwanawe mdogo kama shahidi wake.

Mtoto huyo aliiambia mahakama kwamba kaka yake ameitelekeza familia hiyo baada ya kupata kazi katika jiji la Nairobi. **BBC**

# Ukame waua mifugo, wanyamapori Kenya

**NAIROBI,** KENYA

WATU zaidi ya milioni 26 wanahangaika kupata chakula baada ya hali ya ukame kulikumba eneo la pembe ya Afrika.

Nchi zinazokabiliwa na ukame ni pamoja na Kenya, Somalia na Kusini mwa Ethiopia, ambako kumeshuhudiwa mfululizo wa msimu wa kiangazi na inatarajiwa hali hiyo kuendelea hadi katikati ya mwaka ujao.

Imeelezwa ukame umeathiri pia mifugo na wanyamapori na kusababisha kupoteza maisha kwa kukosa chakula na maji.

Mji wa Wajir uliopo kaskazini mashariki mwa Kenya, umeathiriwa zaidi na ukame. Maofisa walisema kuna idadi kubwa ya mifugo imekufa na inakisiwa asilimia 70 ya ng'ombe na asilimia 60 ya mbuzi wameangamia kutokana na ukosefu wa malisho, maji na magonjwa ya mifugo.

Shirika la Habari la Uingereza (BBC) lilionyesha mizoga ya ng'ombe, mbuzi na twiga ikiwa imetapakaa kando ya barabara kusini mwa mji wa Wajir . **BBC**



Mzoga wa Twiga ukiwa umelala chini kando ya barabara ya kwenda mji wa Wajir nchini Kenya, baada ya ukame kuathiri wanyamapori wanaopatikana katika hifadhi mbalimbali nchini humo. **(PICHA: BBC)**

## Chanjo za Pfizer, Moderna zaonyesha kuhimili corona

**LONDON,** UINGEREZA

CHANJO za Covid-19 aina ya Pfizer na Moderna ambazo zinatumiwa nchini Uingereza kama chanjo za nyongeza, zinaelezwa kutoa kinga bora zaidi kulingana na majaribio saba tofauti yaliyofanywa nchini humo.

Jaribio hilo ni utafiti wa kwanza wa jinsi chanjo ya nyongeza ya Covid inavyofanya kazi vizuri na kuhalalisha uamuzi wa mapema wa Uingereza kutumia chanjo hizi mbili kwa nyongeza.

Chanjo zote zilizojaribiwa ziliongeza kinga dhidi ya Covid kwa kiwango fulani.

Watafiti walisema kulikuwa na ishara zinazoashiria kwamba chanjo hizo za nyongeza zingelitoa matokeo mazuri.

Matokeo hayo yanaonyesha hata usambazaji wa chanjo umekwenda mbali zaidi, kwani hata kipimo cha nusu cha Pfizer kinaweza kutumika na kuongeza idadi ya watu watakaopatiwa chanjo ya nyongeza.

Majaribio yanayofikiriwa kuifanya Uingereza kuagiza dozi zaidi ya milioni 114 za chanjo ya Pfizer na Moderna kutekelezwa katika kipindi cha miaka miwili ijayo.

Chanjo za nyongeza zinaweza kupunguza hatari ya kuambukizwa virusi kwa asilimia zaidi ya 93.

Watu wazima wote walio na umri wa zaidi ya miaka 18 nchini Uingereza wanashinikizwa kupewa chanjo ya nyongeza ya Pfizer au Moderna, huku wanasayansi wakipata maelezo zaidi kuhusu kirusi kipya cha Omicron. **BBC**

## Marekani yatia shaka majeshi ya Urusi

**WASHINGTON,** MAREKANI

MKUU wa majeshi wa Marekani, Jenerali Mark Milley amesema nchi yake inafuatili viashiria na tahadhari zinazohusiana na shughuli za jeshi la Urusi karibu na Ukraine.

Hata hivyo, alisema kuna wasiwasi mkubwa katika wakati ambao Urusi inazidi kuwa na msimamo wa vitisho katika mpaka wa nchi hizo mbili.

Jenerali Miley, alikataa kubashiri kuhusu aina ya hatua ambayo Marekani inaweza kuchukua katika tukio la uvamizi huo unaofanywa na Urusi.

Milley, katika baadhi ya matamshi yake ya kina juu ya mzozo huo, alisisitiza umuhimu wa uhuru wa mamlaka ya Ukraine kwa Marekani na jumuiya ya kujihami ya NATO.

Ukraine ilisema kuwa Urusi imekusanya zaidi ya wanajeshi elfu 90 karibu na mpaka wake, lakini Urusi imepuuza shutma hizo za kwamba inajiandaa kwa shambulio dhidi yake.

**DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**FIDELIS LOSERIAN OLEKASHE.**

Mtajwa hapo juu amepotelewa na passport iliyokuwa na no. **AB 771558** iliyotolewa na makao makuu ya Uhamiaji Tanzania tarehe 13 Nombemba mwaka 2015. Kwa yoyote mwenye taarifa ya upotevu huo atoe taarifa katika kituo chochote cha polisi.Taarifa imetolewa Polisi tarehe 21.Juni 2021 yenye kumbukumbu **RB No.ARU/RB/373839/2021**

116599202

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MUHAMMAD SHAFI RAFI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 798 DDZ – TOYOTA RAUM.** Chassis namba NCZ200053351. Engine namba **3NFE214578.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KW/RB/5615/2021.**

116599002

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**CHRISTIAN SOLOMON SWILLA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.652 DET** AINA YA BMW. CHASSIS NAMBA **WBAAL32050FH72307** ENGINE NAMBA **194E5316924.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/573433/2021.**

116599102

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NDIMBAYE ABEID BWELA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye jina **ELINA NZIKU KAYANDA** aina ya **TOYOTA LANDCRUSER** namba za usajili **T484 AMC.** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi. **DOD/DOD/RB/570447/2021.**

116598702

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ISSA SELEMANI CHABU** Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T830DLC** yeyote atakae iyona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba **0755-753075 DSM /PHQ/RB/570067/2021**

116599302

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **THOMAS RWIZA MUTAGALANJURWA** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya pikipiki aina ya Bajaj Boxer yenye namba za usajili **MC 400 CFE,** namba za injini **DUZWKM6286** na Chassis namba **MDLA18AY6KWM93505.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **KAG/BUK/RB/571431/2021.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi au apige simu namba **0765721385.**

116599402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**
**MAOMBI MADOGO NAMBA 566 YA 2021**

**SILIM AHMED SILIM.............................................. MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**PETER SEMLANGWA EDGA.............................. MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**
**PETER SEMLANGWA EDGA**

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na nyumba la wilaya ya morogoro tarehe 4/01/ 2021 mbele ya mwenyekiti M. KHASSIM wewe mwenyewe binafsi au mtume mwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi ya mepangwa kutajwa. Endapo hutahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi

Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 02 mwezi Desemba 2021.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MOROGORO.

116599502

**Uza,**

**Chenye Thamani Kubwa Kwa**

**Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**

**Mikocheni Industial Area,**

**Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

DIANA ni msichana mrembo kwa maana halisi ya urembo. Na mwenyewe alijijua kuwa ni mzuri wa shani. Aliwababaisha, kuwaliza na kuwatia wazimu wanaume wengi ambao walikutana nao, au hata kupishana tu. Wengi walimkimbilia. Wakamtongoza, kumtaka kimapenzi. Wapo waliotaka kumuoa kabisa. Hata hivyo yeye mwenyewe hakujua ni mwanaume gani anayempenda kwa dhati. Alichojua wengi wanamfuata kama nyuki wafuatavyo ua zuri la waridi. Aliacha muda uongee. Alijua mwisho wa siku atajulikana ni nani anayependa uzuri na urembo wake na nani nampenda kwa dhati. Alayempenda yeye kama yeye na si urembo wake. Fuatilia mtiririko huu wa riwaya hii kabambe, yenye kusisimua na mafunzo kwa jamii.

# Operesheni Namba Moja-3

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

"Naitwa afande Marco."

"Mimi naitwa Diana, nadhani jina langu unalijua kwa sababu jana uliliandika kwenye kitabu chako."

"Ni kweli."

Tinted ilikuwa ni moja ya hoteli za kisasa. Kwa upande wa mbele kulikuwa na mahema ya kisasa na watu walionekana kama wako nje hivi. Lakini wakiwa wamehifadhiwa kwenye mahema, yaliyopambwa na kunakshiwa na urembo mbalimbali.

Watu wenye hela zao kwa sasa ndiyo wamekuwa wakikimbilia hapo kutumia. Ukiacha sehemu hiyo, kuna nyumba ya ghorofa moja ambayo ndiyo kuna vyumba vya hoteli hiyo. Chini ya sehemu ambayo watu wanapata vinywaji mbalimbali, na vyakula pia.

Hakuna yoyote kati ya afande Marco na Diana aliyeagiza bia. Kila mtu aliagiza soda.

Hata hivyo wote si kwamba hawanywi bia. Ni mazingira tu yamewafanya hivyo.

Marco alikuja kwa lengo moja tu la kumhitaji msichana huyo, hivyo hakuona ilikuwa ni fursa nzuri ya kunywa bia. Na hata hakutaka kukaa sana sehemu hiyo kwa siku hiyo.

Kwake Diana ilikuwa ni mapema mno. Hakutaka kuonekana anakunywa, hasa kwa mtu mpya ambaye hakujua nini amemuitia. Pia alijua alianza kunywa, umakini wake unaweza kupotea na kukubalia kila jambo analoweza kuambiwa.

"Enhee afande Marco, naona dakika zinazidi kwenda tu, mimi nimekuja hapa mara moja, nyumbani wameshaanza kunipigia simu."

"Ina maana mzee ameshaanza kukupigia simu?"

"Hapana, mimi sijaolewa bado, ila mjomba, unajua naishi kwake kwa hiyo ni lazima nifuate masharti yake, ingawa hanibani, lakini huwezi kuwa unakwenda kwa muda unaoutaka wewe." Alijibu Diana.

Afande Marco aliona kabisa kuwa Diana ni mmoja wa wasichana waliolelewa kwenye misingi bora ya nidhamu.

"Sikiliza Diana, mimi tangu ulipokuja jana kituoni, moyo wangu umetokea kukupenda sana. Nimejaribu kutaka kuvumilia, lakini nimeshindwa. Ndiyo maana uliona nilichukua namba yako. Niliichukua kimkakati na wala haikuwa ni lazima mimi kufanya vile, lakini nilitaka tu njia ya kukufikishia ujumbe wangu."




**"Mama yangu weee." Ilikuwa ni sauti ya Diana ambaye alipigwa kikubwa, mkoba ulikuwa kwenye meza, mwizi alikuwa na shabaha nzuri kwani aliukwapua na kuanza kutimua mbio.**

Diana hakujibu. Akabaki anamuangalia.

"Nakupenda sana Diana. Sijui nifanye nini, lakini ninachoshuru ni kwamba mzigo wa dukuduku nimeutua kwako mwenyewe mhusika, hilo litanipunguzia mawazo." Alisema afande Marco ambaye Diana alimuona tofauti na jana, kwani alikuja na nguo za kiraia tu, tofauti na ilivyokuwa jana yake.

"Sawa mimi nimekuelewa afande, lakini hili ni ombi na mimi nitakwenda nyumbani kutafakari kabla ya kulitolea jibu."

"Nisubiri kwa siku ngapi?" Marco aliuliza.

"Mambo haya hayana siku. Ni kutafakari tu na kuamua, haya ni mambo ya mahusiano ujue, inabidi mtu uwe makini." Diana akajibu kwa namna ambayo haimkatishi mtu tamaa na wala haimpi nafasi ya moja kwa moja kujiona anaweza kukubaliwa.

********************************

Tayari alikuwa kwenye wimbi la mawazo. Alikuwa na wanaume wawili ambao walionekana kumtaka hasa. Chala na afande Marco. "Sasa nimchague nani?" Alijiuliza. Hakupata jibu. Mwenyewe hakuwa na haraka. Muda ndiyo utaongea.

Siku hiyo alikuwa mitaa ya Mwananyamala, akiwa ametoka hospitali kumuangalia mgonjwa.

Akaamua aingie hotelini kupata chakula. "Naomba chips na kuku." Akaagiza.

Wakati anakula, akili yake yote iko kwenye msosi alisikia sauti ambayo si nzito na si nyepesi.

"Samahani dada hapa kuna mtu?"

"Hapana kaka hakuna."

"Naomba nikae."

"Kaa tu."

Hata hivyo Diana alishangaa kidogo kwa yule aliyetaka kukaa karibu naye, kwani kulikuwa na nafasi nyingi za kukaa. Kulikuwa na viti vingi vilivyo tupu.

Ikabidi ainue macho yake kumtazama mtu huyo. Alikuwa ni mwanaume anayekaribia miaka 40. Alikuwa mwembamba mrefu, maji ya kunde.

Alivaa shati la kawaida la mikono mirefu, suruali ya kitambaa na kiatu vyeusi.

"Naomba ugali na nyama ya kuchoma." Aliagiza.

Chakula kilipokuja alimkaribisha Diana.

"Karibu dada."

Diana aliinua tena macho, akatabasamu na kujibu "Ahsante."

Tabasamu lake ni kwamba yeye anakula, lakini jamaa anamkaribisha tena.

"Au chakula ninachokula ndiyo tatizo, maana nyingi kina dada ampendi ugali." jamaa aliendelea kuongea.

Diana akacheka kicheko kifupi "Hapana, mimi huwa nakula sana, ila hata huku nako ule ugali?" Diana alisema sasa kicheko kikahamia kwa yule jamaa.

"Ugali nyumbani siyo na si huku. Huku ni mwendo wa chips tu si ndiyo?"

"Ndiyo hivyo hivyo."

Wakati msichana anayefanya kazi hapo alipokuja kuchukua pesa kwa Diana, jamaa yule alimwambia yeye ndiyo atalipa.

"Nitamlipia dada yangu." Alisema.

Diana hakutia neno, badala yake alishukuru "Ahsante sana kaka yangu."

Ilikuwa ghafla sana. Kuna kijana aliingia ndani akionekana kama anataka kununua au kuagiza chakula, lakini haikuwa hivyo.

Alipora mkoba wa diana na kuanza kukimbia nao.

"Mama yangu weee." Ilikuwa ni sauti ya Diana ambaye alipigwa kikubwa, mkoba ulikuwa kwenye meza, mwizi alikuwa na shabaha nzuri kwani aliukwapua na kuanza kutimua mbio.

Kitendo bila kuchelewa. Jamaa aliyekuwa anakula na Diana naye alitoka spidi pamoja na mwizi nje. Kitendo kile kiliwachanganya watu wote waliokuwa mle ndani wasijue nini kimetokea.

Baadhi walitoka nje kuangalia ni kitu gani kimetokea.

Walichoona na jamaa kumzidi mbio mwizi, kabla ya kumpiga mtama. Mwizi akaanguka chini. Akachukua mkoba na kupiga mateke kadhaa kabla watu hawajafika kuulizia kuna nini.

"Ni mwizi huyu, kapora mkoba wa dada wa watu wakati anakula pale hotelini." Alijibu.

Kilichofuatia ni kipigo kutoka kwa raia mwema.

Jamaa hakuendelea. Alichukua mkoba wake na kumuacha mwizi akiwa mikononi mwa wananchi wenye hasira kali. Akarudi hadi kwenye mgawaha ule. Alimkuta Diana na watu wengine aliowaacha wapo nje. Diana alikuwa analia machozi.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# MINZIRO ATEMA CHECHE, AICHAMBUA SIMBA BARA

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Geita Gold, Fred Minziro amefichua kinachoifanya Simba kupata tabu katika baadhi ya mechi zake za mashindano mbalimbali wanayoshiriki ni kushindwa kucheza vyema kwenye kipindi cha pili kutokana na wachezaji wake kuchoka.

Minziro aliliambia gazeti hili nyota wa Simba wanaonekana kuchoka zaidi baada ya dakika 30 za kwanza na hapo kikosi chao huwa kwenye wakati mgumu.

Kocha huyo alisema amekuwa akiifuatilia Simba tangu kuanza kwa msimu huu na hata alipokuwa akijiandaa kucheza dhidi yao na kugundua mapungufu yao na kusababisha kuisumbua pale walipokutana hivi karibuni.

Alisema tofauti na inavyozungumzwa, kiuhalisia Simba ni timu ya kawaida na haipaswi kuogopewa.

"Simba ni timu kubwa na nzuri kwa hiyo ilikuwa ni lazima niingie kwa tahadhari na nilijua dakika zao ni za mwanzoni tu, mpaka dakika 30 hivi, ikishapita hapo inakuwa ya kawaida tu. Nilijaribu kupambana lakini ilishindikana tukafungwa mabao mawili, baadaye ikabidi tufunguke kama ambavyo tulivyofanya katika misimu kadhaa nyuma nilipoliwa na Mbao FC kama utakumbuka, tukashinda mabao 3-2, lakini makosa madogo yakatufanya tushindwe kupata matokeo mazuri," alisema Minziro.

Msimu huu Simba imekuwa ikionekana kutawala zaidi kipindi cha kwanza, lakini inadorora kipindi cha pili na kuruhusu mashambulizi mengi, kitu ambacho kimewaathiri katika baadhi ya mechi za Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa.

Mabingwa hao watetezi ndiyo timu iliyopata 'pre-season' ndefu zaidi kuliko klabu nyingine za hapa nchini, ilikwenda kuweka kambi Morocco, lakini ilifanya pia 'pre-season' nyingine iliporejea hapa nyumbani.

Katika msimamo wa ligi, mabingwa watetezi, Simba wako katika nafasi ya pili baada ya kufikisha pointi 17 wakati vinara ni Yanga yenye pointi 19.

Timu hizo zinatarajiwa kukutana Desemba 11, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

## Wanamichezo TPA 'waamshwa'

**Na Beatrice Shayo**

HUKU akiwapongeza kwa kuwa mabingwa wa mashindano ya SHIMMUTA, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA), Erick Hamis, amewataka wafanyakazi wa mamlaka hiyo kuwekeza nguvu zaidi katika kufanya kazi zao za kila siku ili kuhakikisha wanafikia lengo la kukusanya zaidi ya Sh. trilioni moja ifikiapo Juni mwakani mwaka 2022.

TPA ilitangazwa kuwa washindi wa jumla baada ya kushinda vikombe 40 katika mashindano ya Shirikisho ya Umma na Kampuni Binafsi yaliyomalizika wiki iliyopita mkoani Morogoro.

Hamis alisema hayo katika sherehe fupi ya kuipongeza timu yao iliyochukua ushindi wa jumla katika mashindano ya SHIMMUTA iliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi.

Bosi huyo alisema kufuatia mafanikio waliyopata katika michezo, umefika wakati muafaka wa kuwekeza nguvu hizo pia katika kuwahudumia wateja wa bandari hasa wakati huu wanaotarajia kuongezeka kwa mizigo.

Aliahidi kuwapa ushirikiano katika maeneo yote yanayohitajika kwa ajili ya michezo wanayoshiriki ndani na nje ya Tanzania huku akiwasisitiza kuongeza juhudi ili kurudisha heshima kwa TPA.

Katika hatua nyingine Hamis alisema kama ambavyo wanatarajia nchi nyingine kuja kujifunza namna TPA inavyofanya kazi, anataka mashirika na taasisi nyingine zijifunze michezo kupitia bandari hiyo.



Mshambuliaji wa Polisi Tanzania, Adam Adam (kushoto), akipambana kuwania mpira dhidi ya beki wa Biashara United katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Ushirika, Moshi hivi karibuni. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

## Tanzanite, Burundi majaribuni Chamazi

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Timu ya Soka ya Taifa ya umri chini ya miaka 20 (Tanzanite), kinashuka kuwavaa Burundi katika mchezo wa kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.

Fainali za U-20 za dunia zinatarajiwa kufanyika mwakani nchini Costa Rica.

Kocha wa Tanzanite, Bakari Shime, alisema wamejiandaa vizuri kuelekea mchezo huo na anashukuru wachezaji wake wote wako fiti kukabiliana na wapinzani wao Burundi.

Shime alisema mechi hiyo itakuwa na ushindani lakini hana hofu kutokana na maandalizi waliyoyafanya ikiwa ni pamoja na kufanyia kazi ubora wa Burundi ili kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika mchezo huo.

**"Tumejiandaa kikamilifu, tu najua Burundi wako vizuri, tulikuwa nao hivi karibuni nchini Uganda kila mmoja wetu tunafahamu ubora na madhaifu ya mwenzake, itakuwa mechi ngumu na ya ushindani mkubwa, kila mmoja anatafuta matokeo mazuri," alisema Shime.**

Nahodha wa Tanzanite, Irene Kisisa alisema benchi la ufundi limemaliza majukumu yake na sasa kilichobakia ni wao wachezaji kutowaangusha Watanzania.

Naye Kocha Mkuu wa Burundi, Daniella Niyibimenya, alisema wamejiandaa vizuri na anaifahamu vyema Tanzanite kwa sababu ya kuiona na kukutana nayo mara nyingi kwenye mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA).

"Hii sio mara ya kwanza kukutana na Tanzania, (Tanzanite) tunaujua ubora wao na tumeshaufanyia kazi, tutahakikisha tunapambana kutafuta matokeo bora katika mchezo wa kesho (leo)," alisema Daniella.

Nahodha wa Burundi, Niyomwugere Peace- Olga, alisema Tanzanite sio timu ya kuibeza na ana imani itakuwa ni mechi yenye ushindani.

## ZISIKUPITE

### CAVANI AITAKA BARCA

MSHAMBULIAJI wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Uruguay, Edinson Cavani mwenye umri wa miaka 34, anataka kujiunga na Barcelona msimu ujao wa joto. **(Times)**

### NEWCASTLE YAJIPANGA

NEWCASTLE inawalenga wachezaji wanne wa England ifikapo Januari, miongoni mwao ni kiungo wa kati wa Manchester United, Jesse Lingard mwenye miaka 28, kiungo wa kati wa Tottenham Harry Winks (25), kiungo wa kati wa Chelsea Ross Barkley (27), na beki wa Atletico Madrid, Kieran Trippier (31). **(Telegraph)**

### CALVERT-LEWIN SOKONI

ARSENAL wanamtaka mshambuliaji wa Everton na England, Dominic Calvert-Lewin mwenye umri wa miaka 24, kwa ajili ya kuchukua nafasi ya mshambuliaji, Alexandre Lacazette (30). **(Mirror**

### TELLES ANUKIA ITALIA

MLINZI wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Brazil, Alex Telles mwenye umri wa miaka 28, ananyatiwa na klabu za Inter na AC Milan zote za Italia. **(Sun)**

### ARSENAL, JUVENTUS VITANI

ARSENAL wanachuana na Juventus katika kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Serbia, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 21, kutoka Fiorentina**. (Tuttosport)**

### DORTMUND YAGOMA KUFUNGUKA

KLABU ya Borussia Dortmund imekata kuthibitisha ikiwa mkataba wa mshambuliaji wa Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21, una kipengele cha kumruhusu kuondoka cha thamani ya kati ya euro milioni 75. **(Sport 1)**

### GUARDIOLA NJIA MOJA

MIPANGO imewekwa wa Pep Guardiola kuwa Kocha mpya wa New York City FC wakati mkataba wake na Manchester City utakapomalizika ifikapo 2023. **(90min)**

### DIAZ KUTUA LIVERPOOL

LIVERPOOL imehusishwa na uhamishio wa winga wa Porto na Colombia, Luis Diaz mwenye umri wa miaka 24. **(Marca)**

### CONTE SOKONI RASMI

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte anataka kuchukua udhibiti kamili wa mchakato wa kuwasajili wachezaji katika dirisha la Januari kwa ushirikiano na Mkurugenzi wa Michezo, Fabio Paratici. **(Football Insider)**

### AKE ATAKIWA WEST HAM

KLABU ya West Ham inataka kumsajili mlinzi wa Manchester City na Uholanzi, Nathan Ake mwenye miaka 26. **(90min)**

### TORRES KUONDOKA CITY

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Hispania, Ferran Torres mwenye umri wa miaka 21, ameomba kuondoka Manchester City na amefikia mkataba wa miaka mitano na Barcelona. **(Mundo Deportivo)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO AENDELEA KUKIMBIZA ULAYA

●●● Ni baada ya kuweka rekodi ya kufunga mabao 800 huku pia akiwa ndiye...

**MANCHESTER, England**

CRISTIANO Ronaldo amekuwa mchezaji wa kwanza wa soka duniani katika historia kufunga mabao 800 wakati alipoifungia Manchester United magoli mawili katika ushindi wa 3-2 dhidi ya Arsenal, juzi Alhamisi.

Ilikuwa ni jibu la kawaida la Ronaldo kwa mapendekezo ya hivi majuzi kwamba aina yake ya uchezaji inaweza isifanane na mbinu iliyopendekezwa na kocha wa muda anayekuja, Ralf Rangnick, ambaye alikuwa Old Trafford kwa mara ya kwanza tangu kuteuliwa kwake kumtazama Mreno huyo akifikia kiwango hicho cha ajabu.

Na Mjerumani huyo hawezi kushindwa kuvutiwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36.

Mabao mawili ya Ronaldo yalimfanya afikishe mabao 130 katika vipindi viwili tofauti alivyocheza Manchester United, na kuongeza mabao matano kwa Sporting Lisbon, 450 akiwa Real Madrid, 101 akiwa na Juventus na 115 akiwa na Timu ya Taifa ya Ureno.

Ndiye mfungaji bora wa muda wote katika soka ya kimataifa kwa wanaume, katika Ligi ya Mabingwa Ulaya na kwa Real Madrid.

Mfungaji bora wa muda wote wa Ligi Kuu England, Alan Shearer alisema kwenye Amazon Prime Video: "Lazima tukae hapo na kusema 'wow' na kumshangilia kijana huyo.

"Ni dhamira yake. Ni vigumu sana kufika kileleni, lakini inabaki huko pia. Unapaswa kuamka asubuhi na kwenda tena na ulimwengu wote unakutafuta ufanye maonyesho kila wiki. Ni jambo la kushangaza kwa alichokifanya."

Mchezaji mwenzake, Ronaldo pale United na Ureno, Bruno Fernandes aliongeza: "Ajabu. Sote tunajua anaboresha mchezo, mwaka hadi mwaka. Anataka kuendelea kuwa bora na ndivyo alivyofanya. Anajua jinsi ya kujihamasisha."

MECHI KALI
HOME
AWAY
WOLVERHAMPTON
7.18 | 4.78 | 1.41
LIVERPOOL
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom | m-pesa
halopesa
airtel money
EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa
CHEZA USHINDE
JACKPOT
TZS. 735

# USAJILI WA HAALAND KUMTAJIRISHA RANGNICK



**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imeripotiwa watamlipa, Ralf Rangnick bonasi ya Euro milioni 10 kama ataweza kumleta, Erling Braut Haaland pale Old Trafford kabla ya msimu wa 2022/23.

Haaland anatarajia kuachana na Borussia Dortmund msimu ujao akihusishwa na Manchester United, Manchester City, Chelsea, Bayern Munich, Barcelona na Real Madrid.

Ripoti ya hivi majuzi zilidai, Rangnick ambaye amekubali dili la kuwa kocha wa muda wa United kwa msimu uliosalia kabla ya kuchukua nafasi kama mshauri, amedhamiria kumsajili Haaland.

Kwa mujibu wa Bild, United imeahidi kumlipa Mjerumani huyo bonasi hiyo iwapo ataweza kumleta, Haaland Old Trafford kwenye dirisha la usajili la majira ya joto.

Ripoti hiyo inadai uteuzi wa Rangnick ulikuwa sehemu ya "mpango wazi" wa kumsajili raia huyo wa Norway, ambaye amefunga mabao 71 na asisti 19 kwenye mechi 70 alizoichezea Dortmund katika mashindano yote.



# Laporta apambana kumbakisha Dembele

**BARCELONA, Hispania**

JOAN Laporta ametuma ujumbe kwa Ousmane Dembele huku kukiwa na ripoti ya kukwama kwa mazungumzo ya mkataba mpya.

Ousmane atamaliza mkataba wake na Barcelona msimu ujao wa joto, na jinsi mambo yalivyo, anaweza kuondoka klabuni hapo kwa uhamisho huru.

Barca wamedhamiria kukwepa suala la kuondoka bure, wana nia ya kumsainisha winga huyo mkataba mpya mapema zaidi.

Lakini mazungumzo hayajaenda vizuri huku ripoti zikipendekeza jinsi mambo yalivyo, Dembélé ataondoka msimu ujao wa joto.

Barca hawawezi kutoa mshahara ambao nyota huyu anahitaji kwa sababu ya shida ya kifedha waliyonayo, lakini wakati huo huo, Laporta na kocha mkuu, Xavi Hernandez wanapendekeza Mfaransa kuwa ni sehemu muhimu ya mustakabali wa klabu.

"Dembélé ni mchezaji muhimu sana, anaweza kutoa mengi zaidi kwa Barcelona kuliko alivyotoa. Ikiwa ataendelea na sisi, anaweza kufikia kuwa mchezaji wa kumbukumbu," amesema Laporta akinukuliwa na AS.

Nyota huyo amekuwa Barcelona tangu mwaka 2017 aliposajiliwa kwa dili la thamani ya zaidi ya euro milioni 130.

Akiwa na miaka 24, bado kuna imani kwamba anaweza kufikia mafanikio makubwa akiwa hapo Camp Nou.

5,865,580

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 04/12/21 | 18:00 | Blackpool vs Luton Town | 2.70 | 3.14 | 2.55 |
| 02. 04/12/21 | 18:00 | Reading vs Hull City | 2.35 | 3.23 | 2.89 |
| 03. 04/12/21 | 18:00 | Bristol City vs Derby | 2.40 | 3.14 | 2.89 |
| 04. 04/12/21 | 18:00 | Barnsley vs Huddersfield | 2.70 | 3.14 | 2.55 |
| 05. 04/12/21 | 18:00 | Newcastle vs Burnley | 2.24 | 3.31 | 3.21 |
| 06. 04/12/21 | 18:00 | Southampton vs Brighton | 2.42 | 3.30 | 2.90 |
| 07. 04/12/21 | 23:00 | Real Sociedad vs Real Madrid | 3.01 | 3.26 | 2.37 |
| 08. 05/12/21 | 14:30 | Bologna vs Fiorentina | 2.56 | 3.51 | 2.61 |
| 09. 05/12/21 | 16:00 | Rayo Vallecano vs Espanyol | 2.30 | 3.15 | 3.25 |
| 10. 05/12/21 | 17:00 | Lorient vs Nantes | 2.84 | 3.24 | 2.48 |
| 11. 05/12/21 | 17:30 | QPR vs Stoke City | 2.36 | 3.23 | 2.89 |
| 12. 05/12/21 | 19:30 | Aston Villa vs Leicester | 2.55 | 3.35 | 2.70 |
| 13. 05/12/21 | 20:30 | Levante vs Osasuna | 2.45 | 3.20 | 2.95 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 04 - DESEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 1095 | Erzurum BB vs Istanbulspor | 1.85 | 3.52 | 3.62 |
| 13:30 | 2575 | Alanyaspor vs Sivasspor | 2.19 | 3.44 | 3.05 |
| 13:30 | 5546 | Bandirmaspor vs Genclerbirligi | 1.80 | 3.52 | 3.86 |
| 15:00 | 1951 | Veres Rivne vs Dynamo Kiev | 12.48 | 5.18 | 1.21 |
| 15:30 | 5200 | West Ham vs Chelsea | 4.49 | 3.60 | 1.79 |
| 16:00 | 4294 | Sevilla FC vs Villarreal | 1.96 | 3.44 | 3.84 |
| 17:00 | 2697 | Malmo vs Halmstads BK | 1.31 | 4.73 | 7.91 |
| 17:00 | 2819 | AC Milan vs Salernitana | 1.21 | 6.61 | 12.01 |
| 17:30 | 2638 | Arminia Bielefeld vs FC Koln | 3.23 | 3.43 | 2.16 |
| 17:30 | 2792 | Bayer Leverkusen vs Greuther Furth | 1.22 | 6.77 | 9.95 |
| 17:30 | 2973 | Mainz vs VfL Wolfsburg | 2.50 | 3.20 | 2.85 |
| 17:30 | 2981 | Augsburg vs VfL Bochum | 2.33 | 3.28 | 3.03 |
| 17:30 | 5536 | Hoffenheim vs Eintracht Frankfurt | 1.88 | 3.88 | 3.63 |
| 18:00 | 1330 | Aberdeen vs St Mirren | 1.99 | 3.25 | 3.79 |
| 18:00 | 1564 | Newcastle vs Burnley | 2.26 | 3.34 | 3.15 |
| 18:00 | 1747 | Hamilton vs Dunfermline | 2.59 | 3.27 | 2.54 |
| 18:00 | 1840 | Wolverhampton vs Liverpool | 7.18 | 4.78 | 1.41 |
| 18:00 | 1995 | Nottingham vs Peterborough | 1.76 | 3.55 | 4.33 |
| 18:00 | 2382 | St Johnstone vs Ross County | 2.18 | 3.19 | 3.29 |
| 18:00 | 2503 | Hibernian vs Motherwell | 1.82 | 3.51 | 4.15 |
| 18:00 | 2683 | Arbroath vs Raith Rovers | 2.49 | 3.22 | 2.68 |
| 18:00 | 2876 | Blackpool vs Luton Town | 2.75 | 3.09 | 2.55 |
| 18:00 | 3462 | Southampton vs Brighton | 2.44 | 3.21 | 2.96 |
| 18:00 | 3539 | Cardiff vs Sheffield Utd | 3.09 | 3.33 | 2.19 |
| 18:00 | 3727 | Rangers vs Dundee FC | 1.15 | 7.07 | 15.72 |
| 18:00 | 3784 | Millwall vs Birmingham | 2.14 | 3.14 | 3.39 |
| 18:00 | 4138 | Bristol City vs Derby | 2.44 | 3.14 | 2.85 |
| 18:00 | 4894 | Middlesbrough vs Swansea | 2.02 | 3.34 | 3.49 |
| 18:00 | 5339 | Barnsley vs Huddersfield | 2.66 | 3.11 | 2.61 |
| 18:00 | 5500 | Reading vs Hull City | 2.35 | 3.23 | 2.89 |
| 18:00 | 5606 | Blackburn vs Preston | 2.14 | 3.34 | 3.19 |
| 18:00 | 5966 | Morton vs Ayr United | 2.24 | 3.23 | 3.04 |
| 18:15 | 1598 | OH Leuven vs KAA Gent | 3.95 | 3.85 | 1.78 |
| 18:15 | 1960 | Barcelona vs Betis | 1.55 | 4.44 | 5.30 |
| 18:15 | 4287 | Atromitos vs Apollon Smyrnis | 1.95 | 3.12 | 4.15 |
| 18:15 | 4896 | Volos vs Panetolikos | 1.89 | 3.35 | 4.04 |
| 18:30 | 3220 | PSV Eindhoven vs Utrecht | 1.56 | 4.32 | 4.81 |
| 19:00 | 1532 | Marseille vs Brest | 1.59 | 4.16 | 5.15 |
| 19:00 | 4149 | Galatasaray vs Altay | 1.47 | 4.46 | 5.94 |
| 20:00 | 3404 | FC Zurich vs FC Luzern | 1.83 | 3.80 | 3.75 |
| 20:00 | 3613 | Roma vs Inter | 3.59 | 3.69 | 1.96 |
| 20:30 | 1259 | Borussia Dortmund vs Bayern Munchen | 3.67 | 4.36 | 1.78 |
| 20:30 | 2630 | OFI Crete vs Olympiakos | 6.90 | 4.24 | 1.44 |
| 20:30 | 3205 | Watford vs Manchester City | 12.43 | 6.21 | 1.22 |
| 20:30 | 4186 | Atletico Madrid vs Mallorca | 1.33 | 4.91 | 9.42 |
| 21:00 | 4688 | Lille vs Troyes | 1.47 | 4.40 | 6.39 |
| 21:00 | 4704 | Benfica Lisbon B vs Rio Ave | 2.54 | 3.27 | 2.59 |
| 22:45 | 2815 | Napoli vs Atalanta | 2.48 | 3.50 | 2.70 |
| 23:00 | 4233 | Lens vs Paris St Germain | 4.39 | 4.01 | 1.70 |
| 23:00 | 5834 | Real Sociedad vs Real Madrid | 3.16 | 3.26 | 2.29 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# SURE BOY, MORRIS BASI TENA AZAM FC

**Na Dennis Fussi**

KLABU ya Azam FC imetoa tamko rasmi kuhusu sakata la wachezaji, Salum Aboubakar 'Sure Boy', Mudathir Yahya na Aggrey Morris ambao iliwasimamisha.

Wachezaji hao watatu walisimamishwa kwa muda usiojulikana tangu Septemba, mwaka huu kwa utovu wa nidhamu, huku ikidaiwa huenda wakaachwa jumla na klabu hiyo ya jijini Dar es salaam.

Mkurugenzi wa Soka wa Azam, Jonas Tiboroha amesema wachezaji hao huenda wakaondolewa jumla kwenye kikosi na kupewa nafasi ya kujiunga na timu nyingine ndani au nje ya nchi.

Tiboroha alisema katika kipindi hiki ambacho wanaendelea kutumikia adhabu, Azam inaendelea kuwalipa mishahara kama kawaida, lakini benchi la ufundi chini ya Kocha Mkuu, George Lwandamina halina habari nao tena.

"Sidhani kama Sure Boy, Mudathir na Aggrey watakuja kucheza tena Azam, kocha hana mpango nao tena na sisi kama viongozi hatuna habari nao japokuwa wana mikataba ya kuendelea kuitumikia Azam. Tunaendelea kuwalipa mishahara yao kama kawaida mpaka itakapofikia mwisho," alisema Tiboroha.

Azam inashika nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara ikiwa na alama 10, baada ya kucheza michezo saba ya ligi hiyo msimu huu wa 2021/22.



Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia (katikati), akiwa kwenye Mkutano Mkuu wa Baraza la Bodi ya Ligi Nchini uliofanyika mkoani Morogoro jana. Kulia ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa shirikisho hilo, Athumani Nyamlani na Makamu wa Pili, Steven Mnguto. **PICHA: TFF**

# Mtibwa Sugar kurejea Manungu

**Na Dennis Fussi**

KIKOSI cha Mtibwa Sugar huenda kikarudi kwenye Uwanja wa Manungu mwezi huu baada ya kukamilika kwa maboresho ya uwanja kwa asilimia 80.

Uwanja huo ambao ndio nyumbani kwa Mtibwa Sugar ulifungiwa na Bodi ya Ligi Kuu (TPLB), baada ya kukosa vigezo vya kutumiwa katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la FA.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru amesema kwa sasa uwanja wao umefikia hatua nzuri na wanajiandaa kukirejesha kikosi chao nyumbani.

Kifaru alisema uongozi unapambana kukamilisha maboresho hayo na kufikia asilimia 100, ili kuishawishi TPLB kuwapa ruhusa ya kuutumia katika mechi zake za nyumbani.

"Uwanja wa Manungu upo katika hatua za mwisho, tunaamini maboresho yanayofanywa hapa yatafanikisha kikosi chetu kurejea na kucheza hapa katika michezo yetu ya Ligi Kuu na Kombe la Shirikisho," Kifaru alisema.

Baada ya Uwanja wa Manungu kufungiwa, Mtibwa Sugar ilihamia mjini Gairo kwenye Uwanja wa CCM Gairo, kabla ya kuhamishia mawindo yao katika Uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro na baadaye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

# Michezo

Jumamosi Desemba 4, 2021

Nipashe




**Ronaldo aendelea kukimbiza Ulaya**




Wachezaji wa Simba kutoka kushoto, Jonas Mkude, Ibrahim Ajib (katikati) na Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr' wakienda kupanda ndege kuelekea Zambia kwa ajili ya mechi ya marudiano ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Red Arrows itakayochezwa kesho jijini Lusaka. **PICHA: SIMBA SC**

# SIMBA YAFUNGUKA INAKWENDA VITANI

## ●●●Morrison naye ajiandaa kukabiliana na tetesi 'hujuma' za...

**Na Adam Fungamwango**

IKIWA ni mara ya kwanza anakwenda kuwaongoza ugenini wawakilishi pekee wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya kimataifa, Simba, Kocha Mkuu, Pablo Franco amesema timu yake imejipanga vyema kuelekea mchezo huo wa marudiano wa michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Wenyeji Red Arrows ya Zambia watakaribisha Simba katika mechi ya marudiano ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa kesho jijini Lusaka, Zambia.

Kikosi cha mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara, Simba kiliondoka nchini jana asubuhi na kuwasili salama Lusaka kikiwa na msafara wa watu 50.

Pablo aliliambia gazeti hili wanafahamu wanakwenda 'vitani', hivyo wako imara kupambana na Red Arrows kwa ajili ya kuhakikisha wanasonga mbele kwenye michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

"Tumejipanga kivita, tunajua mechi hii ilivyo na umuhimu mkubwa kwetu, tumejipanga kutorudia makosa ya nyuma, tutapambana," alisema Pablo.

Ofisa Habari Msaidizi wa Simba, Ally Shatry 'Chico' alisema wachezaji wa timu hiyo wameondoka wakiwa na morali kubwa ambayo imechangiwa na ushindi wa mabao 3-0 walioupata hapa nchini Jumapili iliyopita.

"Tumeondoka nchini tukiwa makini na tumejiandaa kikamilifu, tumeondoka na watu 50, kati ya hao, wachezaji ni 25 na waliobakia ni benchi la ufundi, viongozi na maofisa wengine wa klabu, lakini juzi kuna mashabiki wetu takribani 45 walitangulia, hatuna wasiwasi, najua kuna Watanzania wengi huko wataungana pia na sisi," alisema Chico.

Aliongeza lengo la Pablo ni kusonga mbele katika michuano hiyo, hivyo amewaambia wachezaji wanatakiwa kuwa makini na kujituma, lakini pia wasiidharau mechi au kuona tayari wameshafuzu kutokana ushindi walioupata kwenye mechi ya kwanza.

"Sisi kama Watanzania tunachoomba Simba ifuzu ili nafasi nne ambazo tunazo zibaki pale pale, mechi itachezwa saa tisa mchana kwa za saa za Zambia, lakini nyumbani itakuwa ni saa 10:00 jioni," Chico aliongeza.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez alisema kila kitu kinakwenda kama walivyopanga na wanachotarajia kuwa na mchezo bora ambao utawapeleka hatua ya makundi.

"Ni kweli mechi iliyopita ya Ligi Kuu hatukucheza vizuri, lakini hii inatokana na wachezaji hawakuonekana kuipania, huwa ni tofauti, kuna mechi kama hizi kubwa wachezaji wanapambana na kujituma sana," Barbara alisema.

Wakati huo huo, winga wa timu hiyo, Bernard Morrison, ameonekana kuwa na wasiwasi wa kutokea kwa 'hujuma' dhidi yake kuelekea mchezo huo.

Morrison akiwa kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa jijini huku amevaa barakoa alisema anajilinda mwenyewe kabla ya wapinzani wao hawajasema ana virusi vya UVIKO-19 akifika Lusaka.

Kauli hiyo ya Morrison imetokana na kuwapo kwa tetesi za nyota watatu wa Simba akiwamo, Aishi Manula na Meddie Kagere kuandaliwa mkakati wa kuwakuta na UVIKO-19 ili wasicheze mechi hapo kesho.

Morrison ndiye aliyefunga mabao mawili na kutoa pasi ya bao moja, lililofungwa na Meddie Kagere katika mechi ya kwanza dhidi ya Red Arrows.

# Yanga moto

**Na Saada Akida**

KUELEKEA mechi ya watani wa jadi nchini, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi amesema haoni sababu itakayoizuia timu yake kuondoka na pointi tatu kwenye mchezo huo utakaochezwa Desemba 11, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Yanga yenye pointi 19 itashuka dimbani ikiwa ndio vinara wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara wakati mabingwa watetezi, Simba wanafuatia kwenye msimamo wakiwa na pointi 17.

Akizungumza na gazeti hili, Nabi alisema Yanga imejipanga kuendeleza rekodi ya kutopoteza mechi yoyote ya ligi msimu huu kwa sababu wanataka kufikia malengo waliyojiwekea.

Nabi alisema ili ishinde taji la ligi, ni lazima ipate ushindi katika mechi nyingi, ikiwamo dhidi ya wapinzani wao.

"Hesabu za ubingwa zitaeleweka kukamilika kama tutashinda, hawa ndio wapinzani wetu, hutakiwi kumwachia pointi mshindani, tunahitaji pointi za mechi hiyo, najua hawatuwezi," Nabi alisema.

Kocha huyo aliongeza anahitaji kila mchezaji aongeze bidii hasa kutumia vizuri nafasi ambazo watazitengeneza.

"Tunahitaji kuwa makini pia, kutopoteza nguvu ambazo tunatumia pale tunapomiliki mpira, kikubwa timu zote zinafahamiana, nimeangalia wanavyocheza na naamini wao pia wametuangalia, hautakuwa mchezo rahisi kwa yoyote," alisema kocha huyo.

Hata hivyo tayari Simba ambayo kesho itashuka ugenini Zambia kuwavaa Red Arrows katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika, imelalamika ratiba imewabana tofauti na ukiwalinganisha watani zao Yanga ambao walitolewa mapema kwenye michuano ya kimataifa msimu huu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >